JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2022

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2022

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

*Kimechapishwa na*:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es salaam, Tanzania

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO


DIBAJI .... iv

1.0 UTANGULIZI .... 1

2.0 UCHAMBUZI WA KILA SWALI .... 3

2.1 Sehemu A: Kuchagua Jibu Sahihi na Kuoanisha .... 3

2.1.1 Swali la 1: Kuchagua jibu sahihi .... 3

2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu .... 12

2.2 Sehemu B: Majibu Mafupi .... 16

2.2.1 Swali la 3: Kumjua Mwenyezi Mungu .... 16

2.2.2 Swali la 4: Fiqh .... 20

2.2.3 Swali la 5: Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu .... 23

2.2.4 Swali la 6: Qur'an .... 27

2.2.5 Swali la 7: Sunna na Hadithi .... 30

2.2.6 Swali la 8: Historia Katika Uislamu .... 35

2.2.7 Swali la 9: Bara Arab Zama za Jahiliyyah Karne ya 6 A.D .... 38

2.3 Sehemu C: Insha .... 42

2.3.1 Swali la 10: Nguzo za Uislamu .... 42

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA .... 47

4.0 HITIMISHO .... 48

5.0 MAPENDEKEZO .... 48

Kiambatisho Cha Pekee .... 49

## DIBAJI

Taarifa hii ya uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) 2022 somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu inatoa mrejesho kwa wadau kuhusu ufaulu wa wanafunzi katika upimaji wa somo hili na kubainisha sababu mbalimbali zilizochangia katika ufaulu huo.

Uchambuzi uliofanywa katika taarifa hii umebainisha sababu zilizochangia wanafunzi hao kupata alama za juu, wastani na za chini katika kila swali. Aidha, sampuli za majibu ya wanafunzi waliofanya vizuri na wale waliofanya vibaya zimeoneshwa. Sababu zilizowawezesha baadhi ya wanafunzi kujibu maswali kwa usahihi ni pamoja na kuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mada zilizopimwa na kuelewa matakwa ya maswali yaliyoulizwa. Aidha, uchambuzi huu umebaini kuwa baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu maswali kwa usahihi hawakuwa na ujuzi wa kutosha katika mada mbalimbali za Elimu ya Dini ya Kiislamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya maswali.

Baraza la Mitihani lina imani kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wote wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hatimaye kuondoa changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Endapo mapendekezo yaliyotolewa mwishoni mwa taarifa hii yatazingatiwa, ni imani ya Baraza kuwa kiwango cha ufaulu katika somo hili kitaongezeka.

Baraza la Mitihani linatoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika uandishi wa taarifa hii.



Dr. Said Ally Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inahusu uchambuzi wa majibu ya wanafunzi waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) Novemba, 2022 somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Upimaji huu uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo husika wa mwaka 2012 wa kidato cha I na II.

Maswali yaliyotumika katika upimaji huu yaliandaliwa kutoka katika mada kumi ambazo ni: *Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu, Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Nguzo za Uislamu, Qur'an, Sunnah na Hadithi, Bara Arab zama za Jahiliyyah, Fiqh, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu, Historia katika Uislamu, Kumjua Mwenyezi Mungu*. Maswali hayo yaligawanywa katika sehemu tatu; A, B na C zenye jumla ya alama 100. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili (1 na 2), sehemu B ilikuwa na maswali saba (3, 4 ,5, 6, 7, 8 na 9) na sehemu C ilikuwa na swali moja (10). Mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote kumi (10).

Wanafunzi waliosajiliwa kufanya upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2022 walikuwa 93,637 kati yao wanafunzi 85,220 sawa na asilimia 91.01 walifanya upimaji. Idadi hii inaonesha kupungua kwa idadi ya wanafunzi 343 ikilinganishwa na wanafunzi 85,565 waliofanya upimaji wa somo hili mwaka 2021. Kati ya wanafunzi 85,220 waliofanya upimaji mwaka 2022, wanafunzi 41,199 (48.77%) walifaulu katika madaraja mbalimbali. Jedwali lifuatalo linaonesha madaraja ya wanafunzi hao ikilinganishwa na mwaka 2021.

**Jedwali Na. 1: Ulinganifu wa Ufaulu Kati ya Mwaka 2021 na 2022**

| Mwaka | Asilimia ya Ufaulu | Madaraja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | A | B | C | D | F |
| 2021 | 40.23 | 147 | 675 | 8,154 | 25,284 | 50,897 |
| 2022 | 48.77 | 51 | 420 | 9,645 | 31,083 | 43,271 |

Takwimu katika Jedwali Na.1. zinaonesha kuwa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kwa mwaka 2022 kimeongezeka kwa asilimia 8.54 ikilinganishwa na mwaka 2021. Aidha, idadi ya wanafunzi waliofaulu kwa daraja A wamepungua mwaka 2022.

Taarifa hii imechambua majibu ya wanafunzi katika kila swali kwa kuzingatia matakwa ya swali husika, majibu sahihi na majibu yaliyotolewa na wanafunzi katika swali hilo. Aidha, sampuli za majibu ya wanafunzi zimeambatanishwa kwa lengo la kuonesha namna wanafunzi walivyojibu maswali. Taarifa hii imebainisha changamoto zilizowakabili wanafunzi katika kujibu kila swali na kiwango cha ufaulu katika mada mbalimbali zilizopimwa. Aidha, madaraja ya ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 2: Madaraja ya Ufaulu Elimu ya Dini ya Kiislamu**

| Alama | Daraja | Maoni |
|---|---|---|
| 75 - 100 | A | Vizuri Zaidi |
| 65 - 74 | B | Vizuru Sana |
| 45 - 64 | C | Vizuri |
| 30 - 44 | D | Inaridhisha |
| 0 - 29 | F | Hafifu |

Jedwali Na. 2. linaonesha kuwa daraja la juu la ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni A na daraja la chini ni F. Pamoja na kuwa na madaraja matano ya ufaulu kama yalivyooneshwa, taarifa hii itazingatia madaraja matatu katika kuwasilisha ngazi za ufaulu ambayo ni: vizuri, wastani na hafifu. Ufaulu utakuwa dhaifu ikiwa asilimia ya wanafunzi waliofanya vizuri ni 0 hadi 29. Ufaulu ulikuwa wa wastani ikiwa waliofaulu swali ni kati ya asilimia 30 hadi 64 na ufaulu ni mzuri ikiwa ni asilimia 65 hadi 100.

## 2.0 UCHAMBUZI WA KILA SWALI


### 2.1 Sehemu A: Kuchagua Jibu Sahihi na Kuoanisha

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ambapo mwanafunzi alipaswa kujibu maswali yote. Swali la kwanza lilikuwa ni la kuchagua jibu sahihi katika vipengele kumi (i) – (x) ambapo kila kipengele kilikuwa na alama moja. Swali la pili lilikuwa ni la kuoanisha, ambalo lilikuwa na vipengele vitano (i) – (v). Swali hili lilikuwa na alama tano (05) sawa na alama moja (01) kwa kila kipengele. Hivyo sehemu A ilikuwa na jumla ya alama 15.

#### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua jibu sahihi

Katika swali hili wanafunzi walitakiwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo manne waliyopewa (A, B, C na D) kisha kuliandika jibu hilo katika kisanduku. Swali hili lilipima ngazi mbalimbali za umahiri katika mada za *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu*, *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini*, *Nguzo za Uislamu, Qur'an, Bara Arab zama za Jahiliyyah, Sunnah na Hadithi.*

Wanafunzi wote 85,220 (100%) walijibu swali hili. Kati yao wanafunzi 64,624 (75.83%) walipata alama 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani. Wanafunzi 16,164 (18.97%) walipata alama 7 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, wanafunzi 4,432 (5.20%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu dhaifu. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao umeainishwa katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1.*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 94.80 kati ya wanafunzi wote walichagua majibu sahihi na kupata alama 3 hadi 10. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali zilizounda vipengele kumi vya swali hilo. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao katika kila kipengele ni kama ufuatavyo:

Kipengele (i) mwanafunzi alitakiwa kubaini sifa inayomtambulisha mtu aliyeelimika kwa mujibu wa Uislamu. Kipengele hiki kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka sifa muhimu za mtu aliyeelimika kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu. Aidha, wanafunzi weledi katika Dhana ya Elimu katika Uislamu waliweza kuchagua jibu sahihi A *Kutumia maarifa yake ili kufanya mambo kwa ufanisi.* Wanafunzi hao walielewa vema makusudio ya Elimu katika maisha ya Muislamu hivyo waliweza kubaini sifa sahihi ya mtu aliyeelimika.

Baadhi ya wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki walichagua kipotoshi B *Kutumia ujuzi alionao kujinufaisha yeye na familia yake,* na C *Kutumia maarifa aliyonayo ili kutafuta kazi nzuri*. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa Elimu katika Uislamu sio nyenzo ya kutafuta maslahi binafsi au ya familia bali ni nyenzo ya ufanisi katika kufanya mambo. Wengine walichagua kipotoshi D *Kutumia ujuzi alionao ili kupata sifa katika jamii.* Wanafunzi waliochagua kipotoshi D walikosa maarifa ya kutosha juu ya dhana ya kuelimika kama ilivyotafsiriwa katika Uislamu ambapo makusudio yake sio kupata sifa bali kufanya mambo mbalimbali kwa ufanisi bila kutarajia kushukuriwa, kuheshimiwa au kusifiwa na wengine.

Katika kipengele cha (ii) mwanafunzi alitakiwa kubainisha sababu ya Uislamu kufasiri Dini kuwa ni mfumo wa maisha ya mwanadamu. Swali hilo lilipima uelewa wa mwanafunzi kuhusu dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu. Wanafunzi mahiri katika dhana hiyo walichagua jibu sahihi D *Qur'an inatambua uwepo wa Dini zote.* Jibu hilo linabainisha wazi kuwa katika Uislamu dhana ya Dini haifungamani na itikadi au imani fulani bali ni utaratibu wa maisha ambao mtu binafsi au jamii inautumia katika kila hatua ya uhai.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi walichagua kati ya vipotoshi A, B na C. Baadhi yao walichagua kipotoshi A *Inahusisha Imani ya*

*Mwenyezi Mungu* ambacho hakikuwa sahihi kwa sababu imani au itikadi ni nyanja moja tu ya maisha ya mwanadamu hivyo haitoshi kufasiri dhana ya Dini kwa ukamilifu. Wengine walichagua kipotoshi B *Uislamu unalazimisha kusali mara tano,* hoja hii haikuwa sahihi kwa sababu siyo msingi wa tafsiri ya Dini kuwa mfumo wa maisha kwani sala tano zinatekelezwa kwa muda mfupi sana katika saa 24 za siku. Aidha, waliochagua kipotoshi C *Ndiyo tafsiri pekee iliyotolewa na Qur'an,* walionesha kukosa maarifa kabisa katika mada ya Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini kwani kwa mujibu wa Qur'an dhana ya Dini imefasiriwa katika namna nne tofauti ambazo ni pamoja na *Uwezo au mamlaka, Mila au desturi na Siku ya Malipo.* Kwa ujumla wanafunzi waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya msingi katika kuitafsiri dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu.

Kipengele cha (iii) mwanafunzi alitakiwa kuonesha namna ambayo mtu anayesali ataweza kupata utulivu (khushui) katika ibada yake. Kipengele hiki kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kuelewa dhana ya utulivu (*khushui)* katika Sala na namna inavyofikiwa. Wanafunzi mahiri katika Fiqhi ya Sala waliweza kuchagua jibu sahihi C *Ikiwa atahudhurisha mawazo yake ndani ya Sala,* wanafunzi hao walifahamu kuwa kuhudhurisha mawazo na kuzingatia nafasi yako mbele ya unayemuelekea ndio njia kuu ya kupata utulivu katika ibada.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya *Khushui* katika ibada hivo walijibu kutokana na mitazamo mbalimbali ya kijamii. Waliochagua kipotoshi A *Iwapo atasikiliza Qur'an vizuri hata kama hajui maana yake,* walishindwa kujua kuwa usikivu ni sifa inayoendana na kujua maana, hivyo mwanadamu hawezi kupata utulivu katika jambo ambalo hajui maana yake. Waliochagua kipotoshi B *Endapo atasali katika sehemu nzuri na yenye hewa ya kutosha,* walishindwa kuelewa kuwa ibada ya Sala inamlazimu mwanadamu kuitekeleza muda wote wa maisha yake madamu yupo hai. Sala ni miongoni mwa njia kubwa za kutafuta faraja au amani katika nafsi ya mja akiwa katika hali yoyote ya kimaisha, hivyo mabadiliko ya kimazingira sio kigezo cha msingi katika kupata utulivu katika ibada hii. Wanafunzi wengine walichagua herufi D *Endapo atarefusha Sujuud (sijda) katika rakaa,* ambayo pia haikuwa sahihi kwa sababu *Sijda* ni kitendo kimoja kati ya vitendo vingi vinavyokamilisha ibada ya Sala. Vilevile,

walishindwa kuelewa kuwa *khushui* ni hali ya kiakili zaidi kuliko mwili na vitendo.

Katika kipengele cha (iv) mwanafunzi alitakiwa kubaini maana au ufafanuzi unaotosheleza kutoa tafsiri sahihi ya Shahada ya pili. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kutumia maarifa kuhusu nguzo ya kwanza ya Uislamu na maana zake. Wanafunzi weledi katika mada ya Shahada waliweza kuchagua jibu usahihi B *Nashuhudia kuwa Muhammad (S.A.W) ni Mtume wa Allah (S.W)* wanafunzi hao walielewa kuwa maana hii inatafsiri vema matamshi yaliyopo katika Shahada ya pili bila kuongezeka au kupungua kwa maneno.

Wanafunzi waliochagua vipotoshi katika kipengele hiki walionesha wazi kuwa walikosa maarifa ya kutosha kuhusu Shahada na maana zake kwasababu hiyo walishindwa kubaini jibu sahihi. Miongoni mwao walichagua kipotoshi A *Nashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah (S.W)* na C *Nashuhudia kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja tu na asiye mshirika* ambapo vyote viwili vinatoa tafsiri sahihi ya Shahada ya kwanza. Wengine walichagua kipotoshi D *Nashuhudia kuwa Muhammad (S.A.W) ni Mtume pekee wa Allah (S.W).* Wanafunzi hao walishindwa kubaini kuwa Mtume Muhammad (S.AW) ni miongoni mwa Mitume wengi waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu hapa duniani hivyo hakuwa Mtume pekee.

Kipengele cha (v) mwanafunzi alitakiwa kubainisha mazao ambayo ni wajibu kutolewa Zakat ikiwa yamefikia *Nisab* kati ya Machungwa, Zabibu, Mpunga, Maembe na Mahindi. Kipengele hiki kilipima uwezo wa kuchambua mazao yanayostahiki kutolewa Zakat ambapo wanafunzi mahiri katika mada ya Zakat waliweza kuchagua jibu usahihi C *Mahindi, mpunga na zabibu.* Wanafunzi hao walielewa kuwa ibada ya Zakat katika kilimo imebainishwa kwa mazao maalumu na kwamba mazao mengine yaliyotajwa yataingia katika hesabu ikiwa yatalimwa kibiashara na yatahesabiwa katika mlango wa Zakat ya biashara tofauti na Zakat ya mazao.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kubaini mazao stahiki kwa ibada ya Zakat, walichagua kati ya vipotoshi A, B na D. Katika vipotoshi vyote A *Zabibu, mpunga na maembe,* B *Zabibu, maembe na mahindi* na D *Mahindi, maembe na zabibu.* Wanafunzi hao hawakufahamu kuwa maembe hayahusiki katika kutolewa Zakat ya mazao.

Katika kipengele cha (vi) wanafunzi walitakiwa kubainisha jina la Qur’an linalomaanisha upambanuzi wa haki na batili. Kipengele hiki kilipima umahiri wa mwanafunzi kukumbuka majina ya Qur’an na tafsiri zake. Wanafunzi weledi katika mada ya Qur’an walibaini jibu sahihi B *Al-Furqan*.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi walionesha kukosa maarifa kuhusu majina ya Qur’an na maana zake kwani majina yote yaliyotajwa katika vipotoshi hayakuwa na maana zinazokaribiana na jibu sahihi kwahiyo uchaguzi wao ulisababishwa na ukosefu wa maarifa. Wanafunzi hao walichagua kipotoshi A *Adh-Dhikru*, ni jina la Qur’an lenye maana ya ukumbusho na kipotoshi C *At-Tanzil* ni jina la Qur’an lenye maana ya kitabu ama ujumbe ulioteremshwa (kutoka juu) na katika kipotoshi D *Al-Hukmu*, jina la Qur’an linalomaanisha kitabu chenye mamlaka ya kutoa hukumu juu ya mambo mbalimbali katika maisha ya wanadamu.

Kipengele cha (vii) mwanafunzi alitakiwa kubaini sura za Qur’an zinazotambulika kwa jina la *Al-Mu’awwidhatain*. Katika kipengele hiki mwanafunzi alipimwa uelewa wa majina ya sura za Qur’an na maana zake. Wanafunzi weledi katika majina ya sura mbalimbali za Qur’an waliweza kuchagua jibu sahihi B *Suratul-Naas na Suratul Falaq* kwa kuwa jina *Al-Mu’awwidhatain* lina maana ya “kinga mbili” ambalo ni jina mahususi kwa sura hizo mbili zilizotajwa ambazo ni sura za kujikinga na shari za aina mbalimbali. Wanafunzi hao walionesha kufahamu uhusiano baina ya maana ya jina hilo na sura zilizotajwa.

Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi hawakuelewa uhusiano uliopo baina ya majina ya baadhi ya sura zilizotajwa kwenye vipotoshi walivyochagua. Katika kipotoshi A *Suratul-Naas na Suratul Ikhlas,* kulikuwa na sura Ikhlas ambayo haimo katika *Al-Mu’awwidhatain* na jina lake linaakisi maudhui yake juu ya kumtakasa Mwenyezi Mungu kwa jina na sifa zake. Vilevile, katika kipotoshi C *Suratul Ikhlas na Suratul Nasr* na D *Suratul- Falaq na Suratul Nasr* imeongezeka sura Nasr ambayo jina na maudhui ya sura hiyo yanaenea dhana ya ukombozi (nusura) au ushindi kwa hiyo inapishana na dhana ya *Al-Mu’awwidhatain*. Kwa ujumla, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki hawakuwa na ujuzi kuhusu maana na majina ya sura mbalimbali za Qur’an.

Kipengele cha (viii) mwanafunzi alitakiwa kubaini msisitizo uliotolewa kuhusu Sunnah kutoka katika aya ya Qur'an inayosema "*Enyi mlioamini! mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume… (47:33).*" Katika kipengele hicho mwanafunzi alipimwa uwezo wa kuchambua ujumbe mahususi uliopo katika aya iliyotajwa na kuonesha nafasi au umuhimu wa Sunnah. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Sunnah na Umuhimu wake waliweza kuchagua jibu sahihi C *Wajibu wa kumfuata Mtume (S.A.W).* Aya hiyo ilionesha wajibu wa waumini kumtii Mwenyezi Mungu (S.W) sambamba na kumtii Mtume (S.A.W) katika maisha yao.

Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu au nafasi ya Sunnah katika Uislamu na wengine walishindwa kuelewa vema matakwa ya swali katika kipengele hiki. Wengine walichagua vipotoshi A *Wajibu wa kumuamini Mwenyezi Mungu* na B *Wajibu wa kumuamini Mtume wa Mungu,* ambapo inaonesha kuwa walishindwa kubaini muktadha wa aya kwa ujumla kwani maagizo ya aya hiyo yameelekezwa kwa hadhira ya waumini. Kwahiyo, halikuwa agizo la kuamini bali wajibu wao baada ya kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Wengine walichagua kipotoshi D *Wajibu wa kujiimarisha katika imani,* somo ambalo halikutajwa katika aya husika na haikuwa mada ya msingi iliyoulizwa katika kipengele hicho, hivyo wanafunzi hao walionesha kutoelewa vema matakwa ya kipengele hiki.

Katika kipengele cha (ix) mwanafunzi alitakiwa kubainisha tofauti kati ya Sunnah na Hadithi kisheria. Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua dhana ya Sunnah na Hadithi kisheria. Wanafunzi mahiri katika mada ya Sunnah na Hadithi waliweza kubaini tofauti kwa kuchagua jibu sahihi A *Sunna ni mwenendo au matendo ya Mtume (S.A.W) ambayo ni sehemu ya Utume wake wakati Hadithi ni simulizi juu ya Sunnah.* Wanafunzi hao walionesha kuwa walielewa msingi unaotofautisha dhana hizo.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hicho waliashiria kukosa maarifa ya kutosha katika mada ya Sunna na Hadithi. Baadhi ya wanafunzi hao walichagua kipotoshi B *Sunna ni simulizi juu ya Hadithi wakati Hadithi ni mwenendo wa Mtume (S.A.W) ambao ni sehemu ya Utume wake,* ambacho ufafanuzi wa dhana hizo ulichanganywa baina ya maana ya Sunna na Hadithi. Wengine walichagua C *Sunna ni matendo*

*yenye kuongeza thawabu na Hadithi ni simulizi za mambo ya kale* ambayo haikuwa sahihi kwa sababu neno Sunna limepewa tafsiri ya kifiqh na Hadithi imefafanuliwa kilugha, hivyo siyo msingi unaotofautisha kisheria. Kundi lingine lilichagua kipotoshi D *Sunna ni mambo madogo ambayo ukiacha hupati dhambi wakati Hadithi ni simulizi za Mitume (A.S) katika Qur'an,* ambacho ndani yake kulikuwa na ufafanuzi wenye mtazamo potofu juu ya dhana ya Sunna. Hivyo waliochagua vipotoshi hivi waliashiria kukosa maarifa ya kutosha kuhusu Sunna na Hadithi.

Kipengele cha (x) mwanafunzi alitakiwa kubainisha jambo lililohesabiwa kuwa ni mkosi (nuksi) miongoni mwa waarabu kabla ya kuja Mtume Muhammad (S.A.W). Kipengele hiki kilipima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka baadhi ya vitendo vya kijahiliya vilivyokuwa vikifanywa na jamii ya waarabu kabla ya kufikiwa na ujumbe wa Uislamu. Wanafunzi mahiri katika mada ya Bara Arab Zama za Jahiliyah waliweza kujibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi A *Familia kupata mtoto wa kike.* Jambo hili ni mashuhuri katika jamii ya Jahiliyya ambapo ilifikia hatua ya kuwazika watoto wao wakike wakiwa hai wakihofia dhana potofu kuwa ni jambo la aibu (fedheha) na mikosi.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Bara Arab zama za Jahiliyyah, hivyo walishindwa kubaini jambo hilo mahususi miongoni mwa jamii ya waarabu. Baadhi yao walichagua kipotoshi B *Unyang'anyi kwa kutumia silaha,* kwani walishindwa kuzingatia matakwa ya swali ambapo jambo hilo halikutazamwa kama ni mkosi kwao ingawa lilikuwa ni miongoni mwa maovu yaliyokuwa yakifanyika. Kundi lingine lilichagua kipotoshi C *Kuvamiwa Al-Kaaba na jeshi la tembo,* tukio ambalo halikuacha ujumbe wa kuwa ni mkosi bali lilithibitisha utukufu wa Al Kaaba baada ya jeshi lililovamia nyumba hiyo kuhalikishwa kabla ya kutimiza azma yao hiyo ovu. Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi D *Mume kurithishwa mke wa ndugu aliyefariki.* Pamoja na kufanyika kwa jambo hili halikuhesabiwa kuwa ni mkosi bali lilifanyika kwa kuwa mwanamke katika jamii ya Jahiliya alihesabiwa kama sehemu ya mali (bidhaa) inayomilikiwa na mume hivyo mume akifariki alirithiwa pamoja na mali zingine alizoziacha mwanaume huyo. Kwa ujumla, maovu yote yaliyotajwa kwenye vipotoshi yalichukuliwa kuwa kawaida isipokuwa kupata mtoto wa kike. Sampuli ya majibu ya wanafunzi katika swali hili ni kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 1.1 na 1.2.

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Sifa gani inamtambulisha mtu aliyeelimika kwa mujibu wa Uislamu?
A Kutumia maarifa yake ili kufanya mambo kwa ufanisi.
B Kutumia ujuzi alionao kujinufaisha yeye na familia yake.
C Kutumia maarifa aliyonayo ili kutafuta kazi nzuri.
D Kutumia ujuzi alionao ili kupata sifa katika jamii.

[A]

(ii) Kwanini Uislamu umefasiri Dini kuwa ni mfumo wa maisha ya wanadamu?
A Inahusisha Imani ya Mwenyezi Mungu
B Uislamu unalazimisha kusali mara tano
C Ndio tafsiri pekee iliyotolewa na Qur'an
D Qur'an inatambua uwepo wa dini zote

[D]

(iii) Ni kwa namna gani mtu anayesali ataweza kupata utulivu (khushui) katika ibada yake?
A Iwapo atasikiliza Qur'an vizuri hata kama hajui maana yake.
B Endapo atasali katika sehemu nzuri na yenye hewa ya kutosha.
C Ikiwa atahudhurisha mawazo yake ndani ya Sala.
D Endapo atarefusha Sujuud (sijda) katika rakaa.

[C]

(iv) Utatumia ufafanuzi gani unaotosheleza kumpa rafiki yako tafsiri sahihi ya Shahada ya pili?
A Nashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah (S.W)
B Nashuhudia kuwa Muhammad (S.A.W) ni Mtume wa Allah (S.W)
C Nashuhudia kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja tu asiye na mshirika.
D Nashuhudia kuwa Muhammad (S.A.W) ni Mtume pekee wa Allah (S.W)

[B]

(v) Bibi Zainab anamiliki shamba lenye machungwa, zabibu, mpunga, maembe na mahindi. Bainisha mazao ambayo anapaswa kuyatolea Zaka ikiwa yamefikia Nisab.
A Zabibu, Mpunga na Maembe
B Zabibu, Maembe na Mahindi
C Mahindi, Mpunga na Zabibu
D Mahindi, Maembe na Zabibu.

[C]

(vi) Jina gani la Qur'an linamaanisha upambanuzi wa haki na batili?
A Adh-Dhikru B Al-Furqan
C At-Tanzil D Al-Hukmu

[B]

(vii) Sura nyingi katika Qur'an zimepewa majina kulingana na mada au maudhui yake. Ni sura zipi zinatambulika kwa jina la *Al-Mu'awwidhatain*?
A Suratul-Naas na Suratul Ikhlas
B Suratul-Naas na Suratul Falaq
C Suratul Ikhlas na Suratul Nasr
D Suratul-Falaq na Suratul Nasr

[B]

(viii) "Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume… (47:33)". Aya hii inatoa msisitizo gani juu ya Sunna?
A Wajibu wa kumuamini Mwenyezi Mungu.
B Wajibu wa kumuamini Mtume wa Mungu.
C Wajibu wa kumfuata Mtume (SAW).
D Wajibu wa kujiimarisha katika imani.

[C]

(ix) Bainisha tofauti kati ya Sunna na Hadithi kisheria.
A Sunna ni mwenendo au matendo ya Mtume (SAW) ambayo ni sehemu ya utume wake wakati Hadithi ni simulizi juu ya Sunna.
B Sunna ni simulizi juu ya Hadithi wakati Hadithi ni mwenendo wa Mtume (SAW) ambayo ni sehemu ya utume wake.
C Sunna ni matendo yenye kuongeza thawabu na Hadithi ni simulizi za mambo ya kale.
D Sunna ni mambo madogo ambayo ukiacha hupati dhambi wakati Hadithi ni simulizi za Mitume (A.S) katika Qur'an.

[A]

(x) Jambo gani kati ya yafuatayo lilihesabika kuwa ni mkosi (nuksi) miongono mwa waarabu kabla ya kuja Mtume Muhammad (SAW)?
A Familia kupata mtoto wa kike.
B Unyang'anyi kwa kutumia silaha.
C Kuvamiwa Al-kaaba na jeshi la tembo.
D Mume kurithishwa mke wa ndugu aliyefariki.

[A]

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 1.

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Sifa gani inamtambulisha mtu aliyeelimika kwa mujibu wa Uislamu?
A Kutumia maarifa yake ili kufanya mambo kwa ufanisi.
B Kutumia ujuzi alionao kujinufaisha yeye na familia yake.
C Kutumia maarifa aliyonayo ili kutafuta kazi nzuri.
D Kutumia ujuzi alionao ili kupata sifa katika jamii.

[ C ]

(ii) Kwanini Uislamu umefasiri Dini kuwa ni mfumo wa maisha ya wanadamu?
A Inahusisha Imani ya Mwenyezi Mungu
B Uislamu unalazimisha kusali mara tano
C Ndio tafsiri pekee iliyotolewa na Qur'an
D Qur'an inatambua uwepo wa dini zote

[ A ]

(iii) Ni kwa namna gani mtu anayesali ataweza kupata utulivu (khushui) katika ibada yake?
A Iwapo atasikiliza Qur'an vizuri hata kama hajui maana yake.
B Endapo atasali katika sehemu nzuri na yenye hewa ya kutosha.
C Ikiwa atahudhurisha mawazo yake ndani ya Sala.
D Endapo atarefusha Sujuud (sijda) katika rakaa.

[ A ]

(iv) Utatumia ufafanuzi gani unaotosheleza kumpa rafiki yako tafsiri sahihi ya Shahada ya pili?
A Nashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah (S.W)
B Nashuhudia kuwa Muhammad (S.A.W) ni Mtume wa Allah (S.W)
C Nashuhudia kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja tu asiye na mshirika.
D Nashuhudia kuwa Muhammad (S.A.W) ni Mtume pekee wa Allah (S.W)

[ A ]

(v) Bibi Zainab anamiliki shamba lenye machungwa, zabibu, mpunga, maembe na mahindi. Bainisha mazao ambayo anapaswa kuyatolea Zaka ikiwa yamefikia Nisab.
A Zabibu, Mpunga na Maembe
B Zabibu, Maembe na Mahindi
C Mahindi, Mpunga na Zabibu
D Mahindi, Maembe na Zabibu.

[ C ]

(vi) Jina gani la Qur'an linamaanisha upambanuzi wa haki na batili?
A Adh-Dhikru B Al-Furqan
C At-Tanzil D Al-Hukmu

[ A ]

(vii) Sura nyingi katika Qur'an zimepewa majina kulingana na mada au maudhui yake. Ni sura zipi zinatambulika kwa jina la *Al-Mu'awwidhatain*?
A Suratul-Naas na Suratul Ikhlas
B Suratul-Naas na Suratul Falaq
C Suratul Ikhlas na Suratul Nasr
D Suratul-Falaq na Suratul Nasr

[ D ]

(viii) "Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume… (47:33)". Aya hii inatoa msisitizo gani juu ya Sunna?
A Wajibu wa kumuamini Mwenyezi Mungu.
B Wajibu wa kumuamini Mtume wa Mungu.
C Wajibu wa kumfuata Mtume (SAW).
D Wajibu wa kujiimarisha katika imani.

[ B ]

(ix) Bainisha tofauti kati ya Sunna na Hadithi kisheria.
A Sunna ni mwenendo au matendo ya Mtume (SAW) ambayo ni sehemu ya utume wake wakati Hadithi ni simulizi juu ya Sunna.
B Sunna ni simulizi juu ya Hadithi wakati Hadithi ni mwenendo wa Mtume (SAW) ambayo ni sehemu ya utume wake.
C Sunna ni matendo yenye kuongeza thawabu na Hadithi ni simulizi za mambo ya kale.
D Sunna ni mambo madogo ambayo ukiacha hupati dhambi wakati Hadithi ni simulizi za Mitume (A.S) katika Qur'an.

[ D ]

(x) Jambo gani kati ya yafuatayo lilihesabika kuwa ni mkosi (nuksi) miongono mwa waarabu kabla ya kuja Mtume Muhammad (SAW)?
A Familia kupata mtoto wa kike.
B Unyang'anyi kwa kutumia silaha.
C Kuvamiwa Al-kaaba na jeshi la tembo.
D Mume kurithishwa mke wa ndugu aliyefariki.

[ C ]

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1.


### 2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu

Swali lilitoka katika mada ya Nguzo za Uislamu katika mada ndogo ya Shahada. Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuoanisha dhana za Shahada zilizokuwa katika orodha A (i) - (v) na asili ya dhana hizo zilizokuwa katika orodha B (A) – (G) kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika jedwali alilopewa. Swali lilipima umahiri wa mwanafunzi kuhusu nguzo ya Shahada na maana zake kama ifuatavyo:

2. Oanisha dhana za Shahada zilizopo katika **Orodha A** na asili ya dhana hizo zilizopo katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi chini ya namba ya kirumi katika jedwali ulilopewa.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Kiingilio katika Dini ya Uislamu | A. Shahada moja |
| (ii) Ahadi ya utii kwa Mwenyezi Mungu (S.W) | B. Kutamka Shahada mbili |
| (iii) Ahadi ya utii kwa Mtume (S.A.W) | C. Ushirikina |
| (iv) Mafungamano ya Allah (S.W) na Mtume (S.A.W) | D. Shahada ya kwanza |
| (v) Kuikanusha Shahada kivitendo katika maisha. | E. Utawa |
| | F. Ishara ya Shahada mbili |
| | G. Shahada ya pili |

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi wote 85,220 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 46,060 (54.05%) walipata alama 4 na 5 ambao ni ufaulu mzuri na 26,726 (31.36%) walipata alama 2 na 3 ambao ni ufaulu wa wastani. Aidha, wanafunzi 12,434 (14.59%) walipata alama 0 na 1 ambao ni ufaulu dhaifu. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2.*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo asilimia 85.41 ya wanafunzi walipata alama 3 hadi 5. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Shahada ambayo iliunda vipengele vyote vitano vya swali hilo. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao katika kila kipengele ni kama ufuatavyo:

Kipengele cha (i) mwanafunzi alitakiwa kubaini njia ya kuingia katika Dini ya Kiislamu ambapo wanafunzi mahiri katika mada ya Shahada walielewa vizuri hoja ya kipengele hicho na kuoanisha kwa usahihi kwa kuchagua herufi B *Kutamka Shahada Mbili.* Wanafunzi hao walielewa kuwa njia ambayo mtu yoyote ataingia katika Dini ya Kiislamu baada ya kuwa na yakini moyoni mwake ni kutamka Shahada mbili mbele ya mashahidi (Waislamu) wengine. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki baadhi yao walichagua herufi A *Shahada moja* na wengine walichagua herufi D *Shahada ya Kwanza.* Hoja hizo mbili hazikuwa sahihi kwa sababu Shahada moja ni sehemu kati ya Shahada mbili na Shahada ya kwanza ni sehemu ya kwanza ya Shahada ambayo ni kumshuhudia Mwenyezi Mungu, hivyo hoja zote mbili hazikamilishi mtu kuwa Muislamu hadi atakapokamilisha Shahada ya pili. Wengine walichagua herufi F *Ishara ya Shahada Mbili* Wanafunzi hao hawakufahamu kuwa *Ishara za Shahada* siyo njia za mtu kuingia katika Uislamu bali ni alama zinazomsaidia kupata ubainifu wa Dini ya Uislamu na itikadi yake.

Kipengele cha (ii), mwanafunzi alitakiwa kubaini ahadi ya utii kwa Mwenyezi Mungu (S.W) inayopatikana katika Shahada. Wanafunzi weledi katika mada ya Shahada waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi D *Shahada ya Kwanza*. Wanafunzi hao walielewa vema kuwa Shahada ya kwanza inabainisha dhana ya utii kwa Mwenyezi Mungu (S.W). Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, miongoni mwao walichagua herufi G S*hahada ya Pili* ambayo haikuwa sahihi kwa kuwa shahada hiyo ni ahadi ya utii kwa Mtume (S.A.W) na wengine walichagua herufi A *Shahada moja*, ambayo pia si sahihi kwa kuwa haibainishi kuwa ni shahada gani mahususi kati ya shahada ya kwanza au ya pili.

Kipengele cha (iii), mwanafunzi alitakiwa kujua ahadi ya utii kwa Mtume (S.A.W) inayopatikana katika Shahada. Wanafunzi weledi katika mada ya Shahada waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi G *Shahada ya Pili*, ambayo tafsiri yake kivitendo ni kuahidi kuwa utamtii Mtume (S.A.W) katika maisha yako yote kwa kuwa umekubali kuwa yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki baadhi yao walichagua kipotoshi D *Shahada ya Kwanza*, ambapo haikuwa sahihi kwa sababu maana yake kivitendo ni kuahidi kuwa mtiifu kwa Allah (S.W). Wengine walichagua herufi E *Utawa* ambayo haikuwa sahihi kwa kuwa Utawa ni aina ya Dini ambayo wafuasi wake wanajitenga na juhudi mbalimbali za kujiletea maendeleo.

Katika kipengele cha (iv) mwanafunzi alitakiwa kubaini mafungamano ya Allah (S.W) na Mtume (S.A.W) kama ilivyo katika tamko la shahada. Wanafunzi mahiri katika mada ya Shahada waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi F *Ishara ya Shahada Mbili*, wanafunzi hao walielewa kwa upana kuwa ukamilifu wa Uislamu wa mtu ni kuamini kwa pamoja jina la Mwenyezi Mungu (S.W) na Mtume wake (S.A.W).

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hicho, baadhi yao walichagua kipotoshi D *Shahada ya kwanza* ambacho hakikuwa sahihi kwani Shahada ya kwanza ni kumshuhudia Mwenyezi Mungu pekee dhidi ya miungu ya uongo na haijaeleza kuhusu utume. Aidha, wanafunzi wengine walichagua kipotoshi E *Utawa* ambayo ni aina ya Dini ambayo wafuasi wake wanajitenga na juhudi mbalimbali za kujiletea maendeleo ili kufanya ibada tu. Hili halikuwa sahihi kwa kuwa halihusiani na dhana ya mafungamano baina ya Allah (S.W) na Mtume (S.A.W).

Kipengele cha (v), mwanafunzi alitakiwa kuoanisha dhana ya kuikanusha Shahada kivitendo katika maisha na matokeo yake.Wanafunzi weledi wa katika mada ya Shahada waliweza kujibu kwa usahihi hoja hiyo kwa kuchagua herufi C *Ushirikina.* Wanafunzi hao walielewa vema tafsiri ya Ushirikina kuwa ni kuishi kinyume na Shahada katika vitendo na maneno. Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, baadhi yao walichagua herufi F *Ishara ya Shahada Mbili*, ambayo ni kinyume na dhana iliyoulizwa jambo lililoonesha wazi kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nguzo ya kwanza ya Uislamu. Sampuli ya majibu ya wanafunzi katika swali hili ni kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 2.1 na 2.2.

**Majibu**

| Orodha A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| Orodha B | B | D | G | F | C |

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 2.

**Majibu**

| Orodha A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| Orodha B | G | F | E | B | A |

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 2.


## 2.2 Sehemu B: Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali saba ya majibu mafupi (3, 4, 5, 6, 7, 8 na 9) ambapo mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote. Maswali hayo yaliandaliwa kutoka katika mada za *Kumjua Mwenyezi Mungu, Fiqh, Mambo ya lazima kufanyiwa maiti wa Kiislamu, Qur'an, Sunnah na Hadith, Historia katika Uislamu* na *Bara Arab Zama za Jahiliyyah karne ya 6 A.D.*

### 2.2.1 Swali la 3: Kumjua Mwenyezi Mungu

Swali lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b) kutoka katika mada ndogo ya *Njia za kumjua Mwenyezi Mungu.* Katika kipengele (a) mwanafunzi alitakiwa kubainisha kwa ufupi sifa tatu za Mitume na kipengele (b) mwanafunzi alitakiwa kueleza kwa muhtasari kazi mbili za Mitume. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua sifa na kazi za Mitume (A.S).


Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 85,220 (100%) walifanya swali hili. Kati yao wanafunzi 41,265 (48.42%) walipata alama 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 24,807 (29.11%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, wanafunzi 19,148 (22.47%) walipata alama 0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3.*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 77.53 ya wanafunzi walipata kati ya alama 3 hadi 10. Ikilinganishwa na asilimia 22.47 waliopata alama za chini.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa, wanafunzi waliofaulu katika swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sifa na kazi za Mitume kama zilivyofafanuliwa na Uislamu na walielewa vema matakwa ya kila kipengele. Katika kipengele cha 3(a) ambacho mwanafunzi alitakiwa kubainisha sifa tatu za Mitume, wanafunzi hao waliweza kubainisha sifa za Mitume kama vile *Walikuwa binadamu kamili, Walikuwa na tabia njema kabisa, Walikuwa na upeo mkubwa wa elimu na Walikuwa wachamungu wa hali ya juu.* Aidha, katika kipengele cha 3(b) ambacho mwanafunzi alitakiwa kueleza kwa muhtasari kazi mbili za Mitume, wanafunzi hao waliweza kueleza kazi hizo kwa ufasaha kama zilivyobainishwa katika Qur'an. Miongoni mwa kazi walizoeleza ni pamoja na: *Kuwafahamisha watu juu ya Allah (S.W) kwa majina na sifa zake, Kuwafahamisha watu kuhusu mambo ya Ghaibu mfano Moto, Pepo, Hesabu, Kufufuliwa n.k, Kuwafahamisha watu juu ya njia sahihi ya kufuata katika kuendea maisha ya kila siku (Dini) ili wafuzu kupata radhi za Allah (S.W) na Kusaidiana na watu wao kuondosha maovu katika jamii.* Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.


3. (a) Bainisha kwa kifupi sifa tatu za Mitume.

(i) Ni wachamungu wa hali ya juu.

(ii) wana elimu ya hali ya juu.

(iii) Ni binaadamu wa kawaida

(b) Eleza kwa muhtasari kazi mbili za Mitume.

(i) kufikisha wahyi kwa wanaadamu; Mitume hawa ni wale waliotumwa na Allah(sw) kufikisha ujumbe wake kwa binaadamu bila kuugeuza.

(ii) kupigania dini ya kiislamu na kuieneza; Hawa ni wale waliotumwa na kuamrishwa kuisambaza dini hii tukufu ya kiislam na kuipambania.

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 3.

Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili, hawakubaini matakwa ya swali hasa katika kipengele cha kwanza na wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Kumjua Mwenyezi Mungu, hivyo walishindwa kujibu swali ipasavyo.


Katika kipengele 3(a) baadhi ya wanafunzi walioshindwa kuelewa swali waliandika kazi za mitume badala ya sifa zao kama ambavyo swali liliulizwa. Miongoni mwa majibu waliyotoa wanafunzi hao yalikuwa; *Mitume ni mijumbe ya Mwenyezi Mungu, Mitume ni watu ambao walioumbwa na Mwenyezi Mungu wenye kutangaza Dini, Mitume ipo ishirini na tano na yote imeumbwa kumtii Mungu*. Wengine walijibu:- *Kuwahimiza jamii kudumu na swala tano, kukataza maovu na kuelimisha umma, kulingania dini au kueneza Dini na kutoa mafunzo juu ya Mwenyezi Mungu*. Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao walishindwa kubaini matakwa ya kipengele hicho, hivyo walieleza kazi badala ya sifa za Mitume.

Vilevile, wapo waliochanganya kati ya sifa za Mitume na sifa za Malaika, ambapo walibainisha sifa kama vile: *Ni viumbe wa kiroho, Ni viumbe wasio na matashi au matamanio ya kibindamu, Mitume hawana jinsia, hawali wala hawanywi na hawakojoi wala hawanyi*. Majibu haya yalitaja sifa za Malaika na kuashiria kuwa wanafunzi hao hakuelewa matakwa ya swali.

Wengine walishindwa kujibu kwa sababu ya kukosa maarifa kuhusu mada husika, hivyo waliandika baadhi ya kazi na vitendo maalumu vya kiibada pamoja na tabia za kijamii. Wanafunzi hao waliandika mambo kama vile; *Kuswali Sunna* ambalo ni jambo la ibada maalumu, *Kuisomesha jamii, kutowa heri na kuepuka shari, kufikisha ujumbe kutoka kwa Allah (s.w) na kutangaza Dini kwa watu kwa ukamilifu* ambazo ni kazi ama wajibu waliopewa, *Mtume alikuwa ni mtu mwenye furaha*, hii ni sifa ya kijamii ambayo si ya kudumu kwa mwanadamu yoyote. Wengine walijibu: *Kutumia maarifa yake ili kufanya mambo kwa ufanisi, kushushiwa Qur'an na Mwenyezi Mungu (S.W).* Vilevile wengine walijibu*: Mwenye kusoma, Mwenye kusimamisha na mwenye kusoma Qur'an kila wakati, Wenye kutimiza vigezo vyote, Anatakiwa awe amefikisha umri unaohitajika na awe ana kila sifa ya Mitume.* Majibu hayo yalionesha kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa ya kutosha katika mada husika.

Katika kipengele 3(b) mwanafunzi alitakiwa kueleza kwa muhtasari kazi za Mitume. Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi walitaja hoja mbalimbali kama vile: *Kupeleka taarifa kwa malaika wa Allah na kuzisambaza kwa maswahaba na kutoa taarifa kwa maswahaba na kuzipeleka kwa Allah*. Mwanafunzi mwengine aliandika: *Kukusanya Hadithi mbalimbali na kuandika madhambi* na mwengine aliandika; *Ahadi na utii kwa Mwenyezi Mungu na kuwa muaminifu na kumtii Mtume (S.A.W), Kuzuia washirikina katika Dini ya Uislamu na kuongoza Elimu ya Dini ya Uislamu katika Mitume ya Allah (S.W)*. Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa kuhusu kazi za Mitume.

Pia, wapo wanafunzi waliojibu sifa za Maswahaba badala ya kazi za Mitume kama vile: *Walikuwa waja wa Mwenyezi Mungu watiifu na walikuwa hawajawahi kumsaliti Mtume hata siku moja walikuwa wanampenda sana Mtume kuliko chochote*. Majibu hayo yaliakisi sifa za wafuasi wa Mtume (S.A.W) badala ya kazi za Mitume. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili wa usahihi.



3. (a) Bainisha kwa kifupi sifa tatu za Mitume.

(i) Mitume hawana jinsia

(ii) Hawali wala hawanywi

(iii) Hawakojoi wala hawanyi

(b) Eleza kwa muhtasari kazi mbili za Mitume.

(i) Kuandika Madhambi – kazi za mitume ni kuandika mambo mabaya na maovu wanayofanya wanadamu katika hii dunia.

(ii) Kukusanya hadithi – wanafanya kazi ya kukusanya hadithi mbalimbali za mitumi na kuzileta kwa kwa waumini yaani waislamu mfano Qur-an tukufu.


Kielelezo Na. 3.2: Sampuli majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

Katika kielelezo Na. 3.2 kipengele 3(a) mwanafunzi ametaja sifa za Malaika badala ya sifa za Mitume na katika kipengele 3(b) mwanafaunzi alieleza kazi za Malaika katika hoja ya kwanza na kazi ya wanazuoni wa Hadithi (Muhadithina) katika hoja ya pili badala ya kazi za Mitume.

### 2.2.2 Swali la 4: Fiqh

Swali lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b) kutoka katika mada ya Fiqh, ambapo katika kipengele cha 4(a) mwanafunzi alitakiwa kutofautisha baina ya Fiqh Ibadat na Fiqh Muamalat na katika kipengele cha 4(b) mwanafunzi alitakiwa kuainisha misingi mitatu ya Fiqh. Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kuchambua aina za Fiqh sambamba na kuainisha misingi yake.

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 85,220 (100%) walifanya swali hili. Kati yao 34,872 (40.92%) walipata alama 0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu dhaifu na wanafunzi 33,872 (39.25%) walipata alama za 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani. Aidha, wanafunzi 16,895 (19.83%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 4. inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 4**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4.*

Chati Na. 4. inaonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 59.08 ya wanafunzi walipata alama kati ya 3 hadi 10 ikilinganishwa na asilimia 40.92 ya wanafunzi wenye ufaulu hafifu (0 hadi 2.5).

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi waliofaulu katika swali hili unaonesha kuwa, wanafunzi hao walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Fiqh na misingi yake. Hivyo waliweza kutumia maarifa yao vema kujibu swali hilo kwa usahihi. Miongoni mwa

waliyoeleza ni pamoja na; *Fiqh Ibadat ni Elimu inayobainisha namna ya utekelezaji wa Ibada maalumu kama vile Sala na Zaka, Funga na Hija wakati Fiqh Muamalat ni Elimu inayobainisha namna ya utekelezaji wa mambo mbalimbali ya kijamii kama vile ndoa na mirathi, biashara, utawala n.k.* Aidha, katika kujibu kipengele cha 4(b) wanafunzi hao walitaja misingi hiyo ya Fiqh ambayo ni: *Qur'an, Sunnah na Ijtihad (Qiyas na Ijmaa).* Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi aliyefaulu.

4. (a) Tofautisha baina ya Fiqh ibadat na Fiqh muamalat.

Fiqh ibadat ni matendo mahususi ya waumini mfano funga, zakah, swala

Fiqh muamalat ni matendo mahusus ndani ya jamii, mfano talaka, ndoa -

(b) Ainisha misingi mitatu ya Fiqh.

(i) Sunnah

(ii) Qur'an

(iii) Ijtihaad

Kielelezo Na. 4.1: Sampuli majibu sahihi ya swali la 4.

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili walishindwa kubaini matakwa ya swali hususani katika kipengele cha 4(a). Wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Fiqh. Kutokana na sababu hizo wanafunzi hao hawakuweza kujibu swali hili ipasavyo.

Miongoni mwa majibu waliyotoa katika kipengele cha 4(a) ambacho walitakiwa kutofautisha baina ya Fiqh ibadat na Fiqh Muamalat yalikuwa; *Fiqh Ibadat ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika Ibada wakati Fiqh Muamalat ni kumpwekesha Allah katika ufalme wake*. Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao walishindwa kubaini matakwa ya kipengele hiki kwani walichanganya dhana ya Fiqh na Tawhiid.


Wanafunzi wengine waliandika; *Fiqh ni Ibada ya kumuabudu Allah na Fiqh Muamalat kumuabudu Allah (s.w)*. Mwingine aliandika; *Fiqh ibada ni Fiqh ya kumuabudu Allah na Fiqh muamalat ni Fiqh ya kumuamini Allah*. Hoja zote zilizotolewa zilionesha kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu Fiqh.

Wengine walichanganya Fiqh ibadat na ufafanuzi wa Sunna katika mtazamo wa ki-Fiqh ambapo walitoa maelezo kuwa; *Fiqh ibadat ukifanya unapata thawabu na ukiacha unapata dhambi wakati Fiqh muamalat ukifanya unapata dhambi na ukiacha unapata thawabu.* Hata hivyo maelezo aliyoyatoa mwanafunzi yalionesha kuwa hakuelewa swali na hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Fiqh na dhana ya Sunna.

Vilevile, mwanafunzi mwingine alitofautisha dhana za Fiqh kwa ufafanuzi kuwa *Fiqh ibadat ni kumpwekesha Allah katika kuabudu na Fiqh Muamalat ni kumpwekesha Allah katika ibada yake.* Maelezo haya yaliashiria kuwa mwanafunzi alishindwa kubaini matakwa ya kipengele hicho na hakuwa na maarifa ya Fiqh kwani alieleza dhana ya Tawhiid badala ya dhana husika.

Katika kipengele cha 4(b) ambacho mwanafunzi alitakiwa kuainisha misingi mitatu ya Fiqh. Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi walitaja nukta mbalimbali kama vile; *Mahala pa kutubu dhambi zako, mahali pakutoa nia ya mwenyezi Mungu na kufundisha jamii kiujumla*, mwingine aliandika; *Imani, kuswali (kusimamisha swala) na kuimarisha imani*. Mwanafunzi mwingine alijibu kuwa; *Kujua hukmu za kiislamu, Kujua sheria za kiislamu na Kujua dini*. Mwingine alijibu: *Kutoa maana ya Qur'an, kusoma Qur'an na kutia nia.* Yupo pia aliyeeleza habari za*: Kumuabudu Allah, kumuamini Allah na kufuata mambo mema*. Vilevile wengine walitaja:- *Swala, Ibada na kitabu.* Baadhi walibainisha:-*Nia, halali na kizuri*. Majibu haya yalionesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa kuhusu mada ya Fiqh.

Wanafunzi wengine walioshindwa katika kipengele 4(b) walichanganya aina za Fiqh na aina za Tawhiid kama walivyofanya kwenye kipengele 4(a). Wanafunzi hao waliandika; *Fiqh Ibada, Fiqh asmaa wasifaat na Fiqh muamalat*. Wengine walichanganya aina za Fiqh na aina za Faradhi kwani waliandika: *Fiqh kifaya, Fiqh muamalat na Fiqh ibada*. Licha ya kuwa walichanganya dhana tofauti katika kujibu lakini pia walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana hizo walizoziandika kwani maelezo yao yalipishana. Pia wapo waliobanisha Nguzo za Uislamu badala ya Misingi ya Fiqh ambayo ni:-*Swala, Kutoa Sadaqat na Kufunga mwezi wa Ramadhani.* Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


4. (a) Tofautisha baina ya Fiqh ibadat na Fiqh muamalat.

Fiqh Ibadat

Ibada inayo a budiwa

Fiqh muamalat

ibada inaya abuaiwa

(b) Ainisha misingi mitatu ya Fiqh.

(i) FiqhQuddusi

(ii) Fiqh Ibadat

(iii) Fiqh muamalat


Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4.

Katika kielelezo Na. 4.2 kipengele cha 4(a) mwanafunzi alishindwa kutofautisha Fiqh Ibadat na Fiqh Muamalat na kuieleza Fiqh kama ndiyo ibada yenyewe. Kadhalika katika kipengele 4(b) mwanafaunzi alitaja aina moja ya Hadithi kisha akazirudia aina za Fiqh kama majibu.

### 2.2.3 Swali la 5: Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu

Swali hili lilitoka katika mada ya Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu katika mada ndogo ya Kumsalia Maiti. Swali lilikuwa na vipengele 5(a) na 5(b). Katika kipengele 5(a) mwanafunzi alitakiwa kuainisha Sunna tano za Sala ya maiti na katika kipengele 5(b) mwanafunzi alitakiwa kupanga katika mtiririko sahihi nguzo tano za Sala ya maiti. Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua nguzo na Sunna za Sala ya maiti kwa mujibu wa Uislamu.

Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 85,220 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 44,563 (52.29%) walipata alama 0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu hafifu. Wanafunzi 20,644 (44.97%) walipata alama 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 2,333 (3.74%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5.*

Chati Na. 5. inaonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 47.71 ya wanafunzi walipata alama kati ya 3 hadi 10 ikilinganishwa na asilimia 52.29 ya wanafunzi wenye alama hafifu (0 hadi 2.5).

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa, wanafunzi waliopata alama za juu katika swali hili walikuwa na uelewa wakutosha kuhusu Sala ya maiti. Katika kipengele cha 5(a) wanafunzi hao waliweza kuainisha kwa usahihi Sunna zinazopatikana katika Sala ya maiti na katika kipengele cha 5(b) waliweza kuzipanga kwa usahihi nguzo zote za Sala ya maiti katika mtiririko stahiki. Katika kipengele cha 5(a), wanafunzi waliainisha kwa ufasaha Sunna za Sala ya maiti kama vile: *Kuanza na Audhubillah kabla ya kusoma suratul Fat'ha, Kusema aamiin baada ya kumaliza suratul Fat'ha, Kuyasema yote yanayosemwa katika Sala hii kimya kimya isipokuwa Imamu atatoa takbira nne na salamu kwa sauti, Kusali kwa jamaa na safu ziwe witiri, Kuwaombea waislamu wote dua pamoja na maiti, Kutoa salamu ya kwanza na ya pili kwa ukamilifu, Imamu kusimama karibu na kichwa cha maiti mwanaume na kusimama karibu na kiuno (nyonga) kwa maiti mwanamke na kumtakia rehma mtume (S.A.W).* Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 5(a).

5. (a) Ainisha Sunna tano za Sala ya maiti.

(i) Kusoma Audhubillahi kabla ya Al-fatiha

(ii) Kusema Amin baada ya Al-fatiha

(iii) Kusoma kimyakimya

(iv) Iswaliwe safu witri

(v) Kumtakia rehma mtume na waislamu wote

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 5(a).

Aidha, katika kipengele cha 5(b) wanafunzi hao waliweza kupanga nguzo za Sala ya maiti katika mtiririko sahihi kama zinavyotekelezwa katika Sala hiyo. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 5(b).

(b) Panga nguzo za Sala ya maiti zifuatazo katika mtiririko sahihi kwa kuandika namba 1-5 chini ya namba ya kirumi katika jedwali ulilopewa.

(i) Kusoma Suratul- Fat-ha.

(ii) Kumsalia Mtume (S.A.W) kama anavyosaliwa katika Sala ya kawaida.

(iii) Nia.

(iv) Kutoa salamu kwa ukamilifu.

(v) Kumuombea dua maiti.

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|
| 2 | 3 | 1 | 5 | 4 |

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 5(b).

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi ulibaini kuwa, wanafunzi waliofaulu kwa wastani katika swali hili alama zao zilitofautiana kulingana na uwezo wao wa kuchambua matendo ya Sunna katika Sala ya maiti na kupanga kwa usahihi nguzo za sala hiyo.


Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili, walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa ya kuhusu Sala ya maiti. Miongoni mwao wapo ambao hawakuelewa vema matakwa ya swali katika kipengele cha 5(a) kwani walieleza wajibu anaostahiki kufanyiwa maiti wa Kiislamu kama vile: *Kuoshwa, Kukafiniwa, Kusaliwa na Kuzikwa.* Majibu haya hayakuwa sahihi kwa

kuwa hayo ni mambo ya lazima kufanyiwa maiti wa Kiislamu na siyo mambo ya Sunna katika kumsalia maiti.

Wengine walishindwa kuelewa matakwa ya kipengele hicho, hivyo waliainisha masharti ya kuosha maiti, namna ya kuosha maiti na masharti ya Sala ya maiti badala ya kueleza Sunna za Sala ya maiti. Majibu yao yalikuwa: *Maiti iwekwe mbele ya wanaosalia, maiti isiwe shahidi, maiti iwekwe juu ya kitanda chenye tobo chini, maiti itasafishwa kucha zake kwa vijiti na maiti itasafishwa kwa kuvaa gloves.*

Vile vile, wengine walitaja nguzo za Sala ya maiti badala ya Sunna za Sala hiyo kama vile: *Nia, kutoa takbira, kumuombea maiti na kumsomea suratul Fat'ha.* Pia, wapo waliotaja masharti ya Sala kwa ujumla kama vile: *Kuwa twahara, Kuwa na stara, iswaliwe msikitini na iswaliwe na watu kuanzia 40.* Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao walishindwa kubaini matakwa ya swali katika kipengele hiki.

Kwa upande mwingine baadhi ya wanafunzi waliandika; *Suratul Fat'ha, Kurukuu ya kwanza, Kurukuu ya pili na Kutoa salamu*. Majibu haya yalionesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa kuhusu Sala ya maiti kwani katika Sala hiyo hakuna Rukuu kama ilivyo katika Sala ya kawaida. Kielelezo Na. 5.3 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 5(a).


5. (a) Ainisha Sunna tano za Sala ya maiti.

(i) kutoa zaka

(ii) Kuwa saidia wajane

(iii) Kuwa saidia watoto yatima

(iv) Kusaidia wagonjwa

(v) Kuwasaidia walemavu wangozi

Kielelezo Na. 5.3: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5(a).

Katika kielelezo namba 5.3 mwanafunzi alishindwa kuainisha Sunna tano za Sala ya maiti badala yake akataja habari za Zaka na makundi ya wahitaji.

Katika kipengele cha 5(b) ambacho mwanafunzi alitakiwa kupanga katika mtiririko sahihi nguzo tano za Sala ya maiti wanafunzi walioshindwa

kupanga kwa usahihi walichanganya nguzo hizo na kuharibu mtiririko wake kwa kuwa walikosa maarifa kuhusu utekelezaji wa Sala ya maiti. Wengine walishindwa kufuata maelekezo ya swali badala ya kuandika majibu yao kwa namba za kiarabu (kawaida) kwenye jedwali walilopewa waliandika kwa namba za kirumi na wengine walirudia kuandika tena nukuu walizopewa na wachache waliandika herufi. Kielelezo Na. 5.4 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kupanga nukuu hizo kwa usahihi katika vipengele vyote.

(b) Panga nguzo za Sala ya maiti zifuatazo katika mtiririko sahihi kwa kuandika namba 1-5 chini ya namba ya kirumi katika jedwali ulilopewa.

(i) Kusoma Suratul- Fat-ha.

(ii) Kumsalia Mtume (S.A.W) kama anavyosaliwa katika Sala ya kawaida.

(iii) Nia.

(iv) Kutoa salamu kwa ukamilifu.

(v) Kumuombea dua maiti.

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|
| iii | i | ii | iv | v |


Kielelezo Na. 5.4: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5 (b).

Pia, katika kipengele (b) mwanafaunzi alishindwa kupanga kwa mtiririko nguzo tano za Swala ya Maiti na pia alipanga kwa namba za Kirumi badala ya namba za Kawaida (Kiarabu).

### 2.2.4 Swali la 6: Qur’an

Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kubainisha kwa kifupi mafunzo manne ya Surat-Nasr kwa jamii ya Kiislamu. Swali lilitoka katika mada ya Qur’an na lililenga kupima umahiri wa kuchambua mafunzo ya Qur’an katika jamii.

Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 85,220 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 72,078 (84.58%) walipata alama 0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu hafifu. Wanafunzi 10,833 (12.71%) walipata alama 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 2,309 (2.71%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 6.*


Chati Na. 6. inaonesha kwamba, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa dhaifu kwa kuwa asilimia 84.58 ya wanafunzi walipata alama 0 hadi 2.5 ikilinganishwa na asilimia 15.42 ya wanafunzi waliofaulu kwa kiwango cha wastani na vizuri. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika swali hili unabainisha sababu mbalimbali zilizosababisha ufaulu huo kama ifuatavyo;

Wanafunzi waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, baadhi yao walionesha kutoelewa matakwa ya swali hali iliyosababisha wanafunzi hao kuandika hoja tofauti na matakwa ya swali. Wengine walionesha kukosa maarifa kuhusu sura hiyo ya Qur'an hivyo walibuni majibu yao. Miongoni mwao, wapo walioandika hoja kama vile: *Sunnat kaburini-ni sunna ambayo unajinyenyekeza mbele za Mungu subuana wataala kutoa sababu zako, Sunat hibatika-kuwa na matatizo meingi kuswali mtume kukaweka shindo zako mbele ya Mtume, Sunati lihaja ni kuamuka saa nane ukatoa toba zako na kusari suna na Sunati shukuru ni sunna ambayo wakati umefunga mwenzi walamazani uweza kushukulu mwenyenzi mungu*. Pia wapo waliojibu: *Kujifunza juu ya malaika na Qur'an zake, kuelimisha waislamu wote, kuwafanya Waislamu wawe na sifa njema ya kumswalia Mtume (S.A.W) na kuwapa mafunzo wale wenye ulemavu na kuwaweka mahali pazuri*. Wengine walieleza nguzo za imani kama vile:- *Kuamini Mwenyezi Mungu, kuamini Mitume ya Mwenyezi Mungu, Kuamini Qadar za Allah (S.W).* Majibu hayo yanaonesha kuwa wanafunzi walikosa maarifa ya

kutosha ya mada ya Qur'an na mafunzo yake, hivyo waliandika hoja ambazo hazikuhusiana na swali.

Wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali husika na kueleza mafunzo ya Sura zingine za Qur'an kama vile; *Tunajifunza kuwa chanzo cha elimu na fani zote isipokuwa zile za ushirikina ni Allah (S.W), inatakiwa kusoma na kutafuta elimu kupata radhi za Allah (S.W), tunajifunza kuwa Mwenyezi Mungu pekee ndiye anayetutoa katika giza na kutupeleka katika nuru, na tunajifunza kuwa Mwenyezi Mungu amemfundisha kwa kalamu.* Majibu haya yaliakisi mafunzo ya Surat Alaq na siyo Surat Nasr.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walitafsiri baadhi ya aya katika sura mbalimbali kama vile Surat Nasr, Ikhlasi na Kaafirun badala ya mafunzo kutoka katika Surat Nasr. Miongoni mwa majibu hayo yalikuwa: *Itakapokuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi, utawaona watu wakiingia katika dini ya Mwenyezi Mungu makundi kwa makundi na tumuombe msamaha Mwenyezi Mungu,* hii ni tafsiri ya Surat Nasr na siyo mafunzo. Vilevile aliandika tafsiri ya baadhi ya aya katika Surat Ikhlasi ambayo ni: *Mwenyezi Mungu ni mmoja tu, mwenyezi Mungu hana mshirika.* Mwingine aliandika tafsiri ya baadhi ya aya za Surat Kaafiruun kama vile: *Enyi makafiri, siabudu mnachokiabudu, wala nyinyi hamuabudu ninaemuabudu, nyinyi mna dini yenu na mimi nina dini yangu.* Wanafunzi hao walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.


6. Bainisha kwa kifupi mafunzo manne ya Surat-Nasr kwa jamii ya Waislamu.

(i) Suratul - Naas na Suratul Ikhlas

(ii) Suratul Ikhlas na Suratul Nasr


(iii) Suratul- Naas na Suratul Falaq

(iv) Suratul -Falaq na Suratul Nasr

Kielelezo Na 6.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 6.

Katika kielelezo Na 6.1 mwanafunzi alinukuu machaguo manne ya majina ya Sura za Qur'an kutoka katika swali la kwanza kipengele cha saba baada ya kushindwa kubainisha mafunzo manne ya Surat – Nasr.

Licha ya kuwa asilimia 84.58 ya wanafunzi walifanya vibaya katika swali hili, walikuwepo pia wanafunzi waliofanya vizuri. Wanafunzi hao (2.71%) walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Qur'an na mafunzo ya sura zilizochaguliwa na waliweza kutambua matakwa ya swali hilo. Aidha, walibainisha mafunzo ya Surat Nasr kwa usahihi na ufasaha, kama vile: *Siku zote nusra na ushindi unatoka kwa Allah, Waislamu hawana budi kufanya juhudi za makusudi za kuusimamisha Uislamu katika jamii kwa mali na nafsi zao, Waislamu hawana budi kumtukuza Allah (S.W) kwa wingi, Kuzidisha kufanya wema, kutoa sadaka, kusali na kadhalika, Mafanikio kwa mtizamo wa Uislamu ni kusimamisha Uislamu katika jamii na sio kuwa na mali au vitu vingi kwa ajili ya starehe na maisha ya dunia, Waislamu hawana budi kumtegemea Allah na kuchunga mipaka yake ipasavyo na Waislamu hawana budi kujiepusha na kujiona na kujifakharisha.* Kielelezo Na 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.


6. Bainisha kwa kifupi mafunzo manne ya Surat-Nasr kwa jamii ya Waislamu.

(i) Nusra na ushindi havipatikani hivi hivi ila kwa uwezo wake Allah (s.w) peke yake.

(ii) Waislamu wote yatupasa kuinusuru na kuipigania dini ya Allah (s.w)

(iii) Dini ya Allah (s.w) ndiyo dini pekee inayoweza kumnusuru mwanaadamu kutokana na mambo mabaya, machafu na maovu.

(iv) Waislamu wote yatupasa kutubu pindi tunapokuwa tumekosea, kwani Allah ndiye pekee anayeweza ~~kumsa~~ kukubali na kuipokea toba ya mja wake.


Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 6.

### 2.2.5 Swali la 7: Sunna na Hadithi

Swali hili lilikuwa na vipengele (a), (b) na (c), kutoka katika mada ya Sunna na Hadithi mada ndogo ya Uchambuzi wa Hadithi za Mtume (S.A.W). Katika kipengele cha 7(a) mwanafunzi alitakiwa kutaja sifa zinazoonekana katika Hadithi aliyopewa zinazothibitisha kuwa Hadithi

hiyo ni sahihi. Kipengele cha 7(b) mwanafunzi alitakiwa kutoa sababu moja inayoonesha daraja la usahihi wa Hadithi hiyo na kipengele cha 7(c) mwanafunzi alitakiwa kubainisha vigezo viwili vinavyofanana kwa Imam Bukhari na Muslim katika ukusanyaji na uandishi wa Hadithi. Swali hili lililenga kupima umahiri wa kuchambua Hadithi mbalimbali za Mtume (S.A.W) ili kubaini usahihi wake.

Takwimu zinaonesha kuwa kati ya wanafunzi 85,220 (100%) waliofanya upimaji huu, wanafunzi 79,400 (93.17%) walipata alama 0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu hafifu. Wanafunzi 5,177 (6.83%) walipata alama 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 109 (0.13%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, kati ya wanafunzi waliokuwa na ufaulu hafifu, wanafunzi 65,817 (77.20%) walipata alama 0. Chati Na. 7 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7.*

Chati Na. 7. inaonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa hafifu kwa kuwa asilimia 93.17 ya wanafunzi walipata alama 0 hadi 2.5 ikilinganishwa na asilimia 6.83 ya wanafunzi waliofaulu. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika swali hili unabainisha sababu mbalimbali zilizosababisha hali hiyo ya ufaulu kama ifuatavyo;

Uchambuzi unaonesha kuwa, baadhi ya wanafunzi waliopata alama za chini katika swali hili walishindwa kubaini matakwa ya swali hasa katika

kipengele cha 7(b) na 7(c) na wengine walikosa maarifa kuhusu Uchambuzi wa Hadithi za Mtume (S.A.W). Kutokana na sababu hizo wanafunzi hao hawakuweza kujibu swali ipasavyo.

Katika kipengele cha 7(a), majibu ya wanafunzi hao yalikuwa: *Kwa sababu kila mtu anatakiwa kuendana na mambo hayo bila kuyafanya*. Mwingine alijibu: *Hadithi hii ni sahihi kwa sababu Mtume ametoa majibu ambayo mtu anaweza kuyatofautisha na kujua maana*. Wengine wakaeleza: *Matini yake yameanza na amesema, Kwa sababu haijaongezwa vitu vya aina ya saivi, Kwa sababu matini yake yana sira la Allah anasema*. Majibu hayo yote yalidhihirisha kuwa wanafunzi hawa walikosa maarifa ya msingi katika uchambuzi wa Hadithi.

Wengine walinakili sehemu ya matini ya Hadithi hiyo kama majibu, mfano: *Mtume (S.A.W) akajibu ni utoe sadaka nawe umzima unataka mali unahofia ufukara na unatarajia utajiri wala usichelewe roho ikafika kwenye koo*. Mwingine akaeleza: *Ni aina ya Hadithi ambayo imepokelewa kutoka kwa Mtume (S.A.W).* Maelezo hayo yanafafanua aina ya Hadithi na sio sababu ya usahihi wake. Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi walishindwa kubaini matakwa ya swali. Kielelezo Na. 7.1(a) kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele cha 7 (a).

(a) Kwanini Hadithi hii ni sahihi?
Kwa Sababu hadith imetoka Kwa mtume
(S.a.w) mwenyewe na matendo aliyoyalithia

Kielelezo Na. 7.1(a): Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika kipengele cha 7(a).

Katika Kielelezo Na. 7.1 mwanafunzi ametoa hoja ambayo haigusi sababu ya msingi ya usahihi wa Hadithi hiyo kwani hata Hadithi za uongo zinasemwa kuwa zimetoka kwa Mtume (S.A.W) hivyo, kunasibishwa jambo lolote na Mtume sio rufaa ya kuthibitisha uhakika wake.

Katika kipengele cha 7(b) wanafunzi walioshindwa walitoa hoja ambazo hazikuwa sahihi, kama vile; *Kwa kuwa imetoka kwa mtukufu wa darja Mtume wetu*, *Kuwa na ukamilifu wa Hadithi*, *Kwakuwa kasema Abu Hurayra*, Wengine waliandika: *Kwa sababu matini yake yameanza na Abu Hurayra (R.A) amesema*, *Ni kwamba kwa kila mtu hana budi kutofanya kinyume na matakwa ya Mwenyezi Mungu kwa kufuata njia sahihi*

*yakumfikia allah*. Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu kategoria za usahihi wa Hadithi. Kielelezo Na. 7.1(b) kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele cha 7 (b).

(b) Toa sababu moja inayoonesha daraja la usahihi wa Hadithi hiyo
Hadith hii ni sahihi kwa sababu mtume ametamka mwenyewe na kumpa mtu bila kupitisha kwa mtuai.

Kielelezo Na. 7.1(b): Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika kipengele cha 7(b).


Katika kipengele cha 7(c) baadhi ya wanafunzi walibuni majibu ambayo hayakuwa sahihi, miongoni mwa majibu hayo yalikuwa;. *Muslim alikuwa akiandika Hadithi kuhusu Mwenyezi Mungu na makatazo yake na Bukhari alikuwa akiandika Hadithi kuhusu Mwenyezi Mungu na makatazo yake*. Mwingine alijibu: *Imam Bukhari ni uandishi ambao toka enzi za manabii hazibadilishwi wala kuongezwa na Imam Muslim ni uandishi ambao kuna baadhi ya Hadithi zimeongezwa maneno*. Mwingine akaeleza kuwa: *Imam Bukhari huyu ni Imam ambae aliyekusanya Hadithi baada ya Mtume na Imam Muslim pia nae vilevile alikuwa ni miongoni mwa maimamu wote wale wale waliokuwa wakikusanya*. Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu Sunna na Hadithi.

Aidha, walikuwepo wanafunzi wachache walioshindwa kubaini matakwa ya swali. Miongoni mwao walieleza baadhi ya simulizi au habari za ukusanywaji wa Qur’an kama vile; *Kupitia maandishi katika majabali na kuhifadhiwa vifuani* badala ya vigezo vinavyofanana kati ya Imam Bukhari na Imam Muslim. Mwingine akaeleza maana ya Hadithi kilugha na umuhimu wa Hadithi kama vile: *Hadith ni habari kwa mtazamo wa Kiislamu na ni muhimu kwa sababu inatoa mafundisho.* Maelezo haya yalikuwa sahihi lakini hayakuakisi muktadha wa matakwa ya kipengele cha 7(c). Kielelezo Na. 7.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele cha 7(c).

(c) Bainisha vigezo viwili vinavyofanana kwa Imam Bukhari na Muslim katika ukusanyaji na uandishi wa Hadithi.
(i) Hadith zinatoka kwa mtume muhamad (S.a.w) pamoja na maelezo yao
(ii)


Kielelezo Na. 7.1(c): Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika kipengele cha 7(c).

Hata hivyo, pamoja na wanafunzi wengi (93.17%) kushindwa kujibu kwa usahihi swali hilo, walikuwepo wanafunzi wachache (0.13%) walioweza kujibu kwa usahihi na kupata ufaulu mzuri. Wanafunzi hao walionesha kuwa na maarifa kuhusu uchambuzi wa Hadithi za Mtume (S.A.W) na walielewa vema matakwa ya swali katika vipengele vyote vitatu. Ingawa wanafunzi hao walipata alama nzuri lakini walishindwa kupata alama zote katika swali hilo. Aidha, katika kipengele 7(a) majibu sahihi yalikuwa: *Hadithi imekidhi vigezo vyote vya usahihi. Mfano uadilifu wa wapokezi, udhibitifu, haijapingana na Qur'an, haijapingana na uhalisia na haijaahidi malipo makubwa sana kwa amali ndogo.* Kielelezo Na. 7.2(a) kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vizuri katika kipengele cha 7(a).


(a) Kwanini Hadithi hii ni sahihi?
kwa sababu hii hadithi ina matini, riwaya, isnadi na rawi ambayo ni sahihi na havi ungumuzi uongo wala uzushi

Kielelezo Na. 7.2(a): Sampuli ya majibu sahihi ya kipengele cha 7(a).

Katika kipengele 7(b) wanafunzi hao walieleza kuwa: *Hadithi ipo kwenye daraja (nafasi) ya kwanza kwa sababu imekubaliwa kwa pamoja na Imam Bukhari na Muslim*. Aidha, kielelezo Na. 7.2(b) kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vizuri katika kipengele cha 7(b).


(b) Toa sababu moja inayoonesha daraja la usahihi wa Hadithi hiyo
Hadithi hii ina usahihi kwa sababu imepokelewa na Bukhari na Muslim.


Kielelezo Na. 7.2(b): Sampuli ya majibu sahihi ya kipengele cha 7(b).

Mwisho, katika kipengele cha 7(c) ambacho mwanafunzi alitakiwa kubainisha vigezo viwili vinavyofanana kwa Imam Bukhari na Muslim katika ukusanyaji na uandishi wa Hadithi, hapakuwa na mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa ukamilifu katika kipengele hiki. Majibu ya kipengele hiki yalikuwa: (*i) Wote walikuwa wakichunguza usahihi wa Hadithi kwa uangalifu wa hali ya juu kwa kufuatilia historia za wapokezi wake kabla ya kuziandika (ii) Wote walizipanga Hadithi zao kwa kuzingatia milango ya Fiqhi na (iii) Wote walikuwa wanachunguza pia Matini ya Hadithi kabla ya kuziandika.*

### 2.2.6 Swali la 8: Historia Katika Uislamu

Swali lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b) kutoka katika mada ya Historia katika Uislamu, mada ndogo ya *Dhana juu ya Historia.* Katika kipengele cha 8(a) mwanafunzi alitakiwa kutofautisha dhana ya Historia kati ya mtazamo wa Kiislamu na Mtazamo wa Kikafiri na katika kipengele cha 8(b) mwanafunzi alitakiwa kubainisha hoja mbili zinazoonesha umuhimu wa kujifunza Historia kwa mujibu wa Uislamu. Swali lilipima umahiri wa mwanafunzi kuchambua dhana ya Historia kwa mujibu wa Uislamu na umuhimu wake katika jamii.


Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi wote 85,220 (100%) waliofanya upimaji huu walifanya swali hili. Kati yao wanafunzi 53,306 (62.55%) walipata alama 0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Wanafunzi 29,785 (34.95%) walipata alama 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 2,129 (2.50%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 8. inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 8**. *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 8.*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 37.45 ya wanafunzi walipata kati ya alama 3 hadi 6. Aidha, wanafunzi hao waliweza kujibu kipengele kimoja kwa ufasaha na kushindwa kujibu kingine.

Wanafunzi asilimia 2.50 waliofaulu katika swali hili (2.50%) walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Historia katika Uislamu na walielewa vema matakwa ya kila kipengele katika swali. Aidha, katika kipengele cha 8(a) ambacho mwanafunzi alitakiwa kutofautisha dhana ya Historia, wanafunzi hao waliweza kuakisi dhana ya Historia kama ilivyofafanuliwa na Uislamu kuwa; Historia kati ya mtazamo wa Kiislamu *ni kumbukumbu ya matendo na matukio katika maisha yote ya mwanadamu, katika jamii yake kwa muda wote uliopita ikihusisha ulimwengu na vyote vilivyomo na muumba mmoja tu mwenye hekima na ujuzi usio na kikomo WAKATI kwa mtazamo wa kikafiri ni kumbukumbu ya matendo ya mwanadamu aidha katika harakati zake za kupambana na mazingira au harakati za kumwezesha kupata mahitaji yake muhimu kutoka kwenye maumbile ya asili, mfano chakula, malazi na mavazi.* Kielelezo Na. 8.1(a) kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefaulu katika kipengele cha 8(a).


8. (a) Tofautisha dhana ya Historia kati ya mtazamo wa Kiislamu na mtazamo wa Kikafiri.
kwa mtazamo wa kiislamu historia ni matukio a mbayo yamepita kuhusu watu waliopita yana yo eleza makosa na namna ya kuyasahihisha kwa kufuata maamrisho ya Allah kwa mtazamo wa makafiri ni matukio yanayo eleza maisha ya mwanadamu yaliyopita

Kielelezo Na. 8.1(a): Sampuli ya majibu sahihi ya kipengele cha 8(a).

Vilevile, katika kipengele cha 8(b) wanafunzi hao waliweza kutoa hoja mbalimbali zenye kuonesha umuhimu wa historia kama vile: *(i) Hutuonesha asili na Hadhi yetu juu ya viumbe vingine hapa duniani na (ii) hutukumbusha lengo la kuumbwa kwetu na namna ya kulifikia (iii) hutuonesha namna Allah alivyotuneemesha ili tuweze kumuabudu ipasavyo (iv) Hutuonesha madhara ya kutofuata muongozo (v) Hutuonesha namna Mitume au Watu wema walivyosimama imara katika kupambana na Dhulma na Watawala madhalimu (vi) Hutupatia fursa ya kujifunza toka kwa Kaumu zilizopita na kuchukua tahadhari kabla hayajatufika yaliyowasibu na (vii) Kujitathmini na kuongeza jitihada za kusimamisha Haki na Uadilifu kama walivyofanya Mitume.* Kielelezo Na. 8.1(b) kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefaulu katika kipengele hicho.

(b) Bainisha hoja mbili zinazoonesha umuhimu wa kujifunza historia kwa mujibu wa Uislamu.

(i) Hutusaidia kujua historia za mitume na kutambua makosa waliyoyafanya na usahihi wake

(ii) Hutusaidia kujua na kusuluhisho matatizo na migogoro ya kisheria ya kiislamu iliyowahi kutokea katika historia iliyopita

Kielelezo Na. 8.1(b) Sampuli ya majibu sahihi ya kipengele cha 8(b).

Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili, baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali hasa katika kipengele cha 8(a). Wengine walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu Dhana ya Historia kwa mujibu wa Uislamu hivyo hawakuweza kujibu swali ipasavyo.

Katika kipengele 8(a) wanafunzi hao walitoa majibu mbalimbali kama vile; *Kwa mtazamo wa Kiislamu Historia ni kumbukumbu za Mitume wakati kwa mtazamo wa kikafiri ni mambo ambayo yanayohusu jamii na makatazo yao,* Mwingine alieleza; *Kwa mtazamo wa Kiislamu inasema kwamba binadamu wa kwanza aliumbwa kwa udongo wakati kwa upande wa kikafiri inasema kuwa binadamu wa kwanza alikuwa ni nyani*. Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa ya kutosha kuhusu Historia katika Uislamu. Wengine walieleza kuwa; *Historia katika kimtazamo wa Kiislamu ni kufatanisha yale mema na mazuri aliyoyatenda Mtume wetu Muhammad na Allah wakati kwa mtazamo wa makafiri wanafatisha yale mabaya aliyoyatenda Mtume wao Issa,* Mwingine alieleza: *Historia katika mtazamo wa Kiislamu inaweza kuwa Historia ya Mtume, Maswahaba au Malaika wakati kwa Mtazamo wa Makafiri unaweza kuwa Historia ya Izraili, Uchawi na Ushirikina*. Majibu haya yaliashiria kukosa maarifa kabisa katika dhana ya Historia katika Uislamu. Kielelezo Na. 8.1(a) kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele cha 8(a).


8. (a) Tofautisha dhana ya Historia kati ya mtazamo wa Kiislamu na mtazamo wa Kikafiri.

Makafiri hupotosha watu kua kutunga dini zao pasipo kufuata utaratibu aliyo uweka Allah (s.w), Mwenye nzimu alimtuma mjumbe wake akasema Jumnyenyeke

Kielelezo Na. 8.1(a): Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika kipengele cha 8(b).

Katika kielelezo Na. 8.1(a) mwanafunzi ameshindwa kutoa tofauti juu ya dhana ya Historia badala yake akatoa hoja dhidi ya makafiri na agizo la utii kwa Mtume.

Katika kipengele 8(b) baadhi ya wanafunzi walioshindwa walitoa hoja ambazo zilikuwa kinyume na matakwa ya swali. Baadhi ya hoja ni*: (i) Kutuonesha kuwa Mwanadamu wa kwanza aliumbwa kwa udongo na maji pamoja na pumzi (ii) mwanadamu ataishi pia atakufa atarudi kuwa udongo vilevile mwanzo (iii) historia za mitume (s.a.w) zilikuwa ni za kweli. (iv)historia za malaika wa Allah zilikuwa ni za kweli(v) Historia za malaika wa Allah zilikuwa zenye unyenyekevu wa hali ya juu na upeo wa Elimu.* Majibu haya yaliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa kuhusu Historia kwa mujibu wa Uislamu Kielelezo Na. 8.2(b) kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hicho.


(b) Bainisha hoja mbili zinazoonesha umuhimu wa kujifunza historia kwa mujibu wa Uislamu.
(i) historia ni masimulizi ya mambo yakare yenye kufundisha au kupotosha
(ii) historia ni masimulizi ya mambo ya kare yaliyo pitaga hapo nyuma


Kielelezo Na. 8.2(b): Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika kipengele cha 8(b).

Katika Kielelezo Na. 8.2(b) mwanafunzi amefafanua dhana ya Historia badala ya kueleza umuhimu wake katika umma wa Kiislamu.

### 2.2.7 Swali la 9: Bara Arab Zama za Jahiliyyah Karne ya 6 A.D

Swali lilitolewa katika mada ndogo ya Kulingania Uislamu Makkah, ambapo wanafunzi walitakiwa kubainisha ishara tano alizooneshwa Mtume (S.A.W) katika Safari ya Israa na Mii’raj ambazo zilimuimarisha katika kazi yake. Swali lililenga kupima uwezo wa kutathmini matukio muhimu yaliyotokea kwa Mtume (S.A.W) katika safari yake tukufu ya Israa na Mii’raj.

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi wote 85,220 waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Kati yao, wanafunzi 75,754 (88.89%) walipata alama 0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Wanafunzi 7,927 (9.30%) walipata alama 3 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 1,539 (1.81%) walipata alama 6.5 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, kati ya waliopata ufaulu dhaifu, wanafunzi 57,355 (67.30%)) walipata alama 0. Chati Na. 9 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 9:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9.*

Chati Na. 9 inaonesha ufaulu wa jumla ulikuwa dhaifu kwenye swali la 9 kwa kuwa asilimia 88.89 ya wanafunzi hao walipata alama 0 hadi 2.5 ikilinganishwa na asilimia 11.11 waliofaulu vizuri.

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi hao ulionesha kuwa, baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Safari ya Israa na Miiraj na wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Miongoni mwa majibu waliyotoa wanafunzi hao ni kama vile: *Watu kuabudu masanamu, mazingira, machafuko na vita, watu kufanya mambo maovu, watu kutofanya ibada na watu walivyotawaliwa na makafiri katika kueneza Dini yao.* Mwingine alitaja; *Alikuwa akimpwekesha Mtume (S.A.W), Alibadili mchanga kuwa chakula kisafi na kitamu, Kuona mwezi wa Ramadhani, Kuona upepo na mvua, Alikuwa anaamini Vitabu vya Mwenyezi Mungu na aliona sehemu atakapofika na familia yake.* Kadhalika mwanafunzi

mwingine alieleza: *Birika ambalo watakutana Waislamu ili kupata maji ya kunywa, Kuongeza chakula kilichokuwa kidogo na kuwa kingi ili kiweze kuwatosha, Kuwaongoza njia na kufika walipoelekeza, Kuwatembeza usiku na mchana bila kusikia uchovu na alikuwa akitoa Zakat kwa Mtume Muhammad (S.A.W).* Majibu haya yanaonesha wazi kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu safari ya Israa na Miiraj hivyo walikuwa wakiandika matukio mbalimbali katika maisha ya Mtume (S.A.W) ambayo baadhi ni ya kweli na mengine ni ya uongo.

Wengine walionesha kushindwa kuelewa matakwa ya swali hilo badala yake walihusisha majibu yao na matukio mengine tofauti. Miongoni mwao walieleza njia za mawasiliano baina ya Mwenyezi Mungu na waja wake, kama vile; *Ilhamu, Ndoto za kweli, Nyuma ya pazia, kupitia Malaika Jibril na kupitia Vitabu vyake Allah (S.W).* Mwingine alieleza matukio yaliyomkuta Mtume (S.A.W) wakati akipokea wahyi wa kwanza, kama vile; *Kubanwa mbavu na Jibril Mtume Muhammad (S.A.W), Mtume kuambiwa asome na Jibril (A.S), kumtokea Mtume pangoni, Mtume kupiga kelele wakati anabanwa mbavu na kufundishwa kusoma Qur'an*. Mwingine akaelezea matukio yaliyojitokeza katika Hijra ya Mtume (S.A.W) kutoka Makka kwenda Madina kama vile; *Kuwalaza Makafiri mpaka asubuhi waliokuwa wakikusudia kumuua, Kuweka utandu wa buibui katika pango walilokuwa wamejificha Mtume na Abubakar, Kutaka kung'atwa na Nge lakini badali yake Abubakar akajikinga na ikamng'ata yeye, Kupewa uwezo wa kufanya mambo kwa siri bila ya makafiri kujua na kuwafanya makafiri kulipa pango kama kwamba hakuna watu waliomo humo*. Wengine walitaja njia mbalimbali za kumjua Mwenyezi Mungu (S.W) kama vile; *Nafasi ya Fitra, Nafsi ya Mwanadamu, Vipaji vya Mwanadamu, Wahyi (ufunuo) na Mazingira*. Majibu haya hayakuwa sahihi kwa sababu hayakuakisi muktadha wa swali ambalo mwanafunzi alitakiwa kueleza ishara alizooneshwa Mtume (S.A.W) katika safari ya Israa na Miiraj.

Kwa ujumla, wanafunzi walioshindwa kujibu swali kwa usahihi walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Kulingania Uislamu Makka na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali. Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.

9. Safari ya Israa na Miiraj ilikusudiwa kumuonesha Mtume (S.A.W) utukufu wa Mwenyezi Mungu (S.W) kupitia ishara zake mbalimbali ili kumuimarisha zaidi katika kazi yake. Bainisha ishara tano alizooneshwa katika kufanikisha makusudio hayo.

(i) Kuswali Swalatano . kutamka Sha hadambili

(ii) Kumuamini Allah

(iii) Kuamini malaika Wake


(iv) Kuamini mitume wake

(v) Kuamini Vitabu Vya Allah

Kielelezo 9.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 9.

Katika kielelezo Na. 9.1 mwanafunzi ametaja nguzo mbili za Uislamu na Nguzo nne za Imani ya Kiislamu badala ya kubainisha ishara tano alizooneshwa Mtume (S.A.W) katika safari yake ya Israa na Mi’raj.

Licha ya kuwa na ufaulu dhaifu katika swali hili, walikuwepo wanafunzi wachache (1.81%) waliofanya vizuri. Wanafunzi hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu safari ya Israa na Miiraj na walielewa vema matakwa ya swali, hivyo waliweza kubainisha ishara mbalimbali alizooneshwa Mtume (S.A.W) katika safari hiyo. Miongoni mwa ishara hizo ni; (i) *Kufika msikiti wa Aqsa ulioko Jerusalem ambao ni Qibla ya kwanza kwa Waislamu tokea kwa Mitume wote wa Bani Israil kabla ya kuamriwa kuelekea Alkaaba katika mji wa Makka,(ii) Mtume (S.A.W) kuwa Imamu wa Mitume wote na kuswali rakaa mbili pamoja nao, hii inaashiria yeye ni kiongozi wa Mitume wote na ulimwengu mzima,(iii) Kupelekwa mahali pa faragha huko mbinguni nakuzungumza na Allah kama alivyozungumza nabii Mussa (A.S),(iv) Kuoneshwa moto na pepo ili kupata yakini zaidi juu ya kuwepo maisha ya akhera, (v) Kukabidhiwa Sala tano za faradhi kwa ajili ya Umma wake, (vi) Idadi kubwa ya Sala kuliko zile zilizofaradhishwa umma zilizopita na (vii) Safari yenyewe kuchukua muda mfupi kuonesha uwezo wa Allah ambapo Mtume alisafiri kwa kutumia mnyama wa miujiza aliyekwenda kasi sana kwa muda wa usiku mmoja tu*. Kielelezo Na 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 9.


9. Safari ya Israa na Miiraj ilikusudiwa kumuonesha Mtume (S.A.W) utukufu wa Mwenyezi Mungu (S.W) kupitia ishara zake mbalimbali ili kumuimarisha zaidi katika kazi yake. Bainisha ishara tano alizooneshwa katika kufanikisha makusudio hayo.

(i) Mtume (s.a.w) kuwaswalisha mitume wengine wote rakaa mbili

(ii) Mtume (s.a.w) alioneshwa pepo na moto dalili hii kuonesha utukufu wa Allah (s.w)

(iii) Kupanda Buraq - Buraq ni mnyama / chombo ambacho kuna kasi ya ajabu hakuna mwenye uwezo wa kukimbia au kumpata.

(iv) Kuondoka usiku na kurudi usiku ule ule.

(v) Kumpa mtume zawadi ya swala 50 na kumpunguzia mpaka kufikia tano

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 9.


## 2.3 Sehemu C: Insha

Sehemu hii ilikuwa na swali moja la insha kutoka katika mada ya *Nguzo za Uislamu,* swali hilo lilikuwa na alama 15.

### 2.3.1 Swali la 10: Nguzo za Uislamu

Swali lilitoka katika mada ndogo ya Kusimamisha Sala Nyakati za Dharura ambapo mwanafunzi alitakiwa kubainisha ruhusa tano zinazoonesha wepesi aliopewa mgonjwa katika kutimiza Sala tano za faradhi. Katika swali hili mwanafunzi alipimwa umahiri wake katika kutathmini mafundisho ya Sala kwa namna yalivyofanywa kuwa mepesi kwa Muislamu akiwa katika hali ya ugonjwa.

Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 85,220 (100%) waliofanya upimaji huu. Kati yao wanafunzi 44,608 (52.34%) walipata alama 0 hadi 4 ambao ni ufaulu hafifu. Wanafunzi 32,599 (38.25%) walipata alama 4.5 hadi 9.5 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 8,013 (9.40%) walipata alama 10 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 10.





**Chati Na. 10:** *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 10.*

Chati Na. 10 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wastani kwa wanafunzi katika swali la 10 kwa kuwa asilimia 47.66 ya wanafunzi hao walipata alama 4.5 hadi 15 ikilinganishwa na asilimia 52.34 waliokuwa na ufaulu hafifu. Tofauti ya alama za wanafunzi hao ilichangiwa na uwezo wao katika kuwasilisha hoja na kuzifafanua kulingana na matakwa ya swali.

Aidha, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Nguzo za Uislamu hususani katika mada ya Kusimamisha Sala nyakati za Dharura na walielewa vema matakwa ya swali, hivyo waliweza kujibu kwa usahihi.

Miongoni mwa ruhusa walizobainisha ni pamoja na; *Mgonjwa ameruhusiwa kutayammam iwapo hawezi kutumia maji kutokana na ugonjwa wake, Mgonjwa ameruhusiwa kuswali akiwa amekaa na kuelekea Qibla, ameruhusiwa kuchanganya Sala, ameruhusiwa kupunguza Sala, mgonjwa ameruhusiwa kuswali akiwa amekaa na kuelekea Qibla, Ikiwa atashindwa mgonjwa ameruhusiwa kusali akiwa ameelekea popote na hata kutayyammam kifikra iwapo hajimudu na hana mtu wa Kumtwaharisha.* Hoja hizi zilibainisha wazi namna ambavyo Mwenyezi Mungu (S.W) ametoa wepesi kwa waja wake katika kutekeleza wajibu aliowapa endapo

watakuwa na dharura. Kielelezo Na 10.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.



10. Bainisha ruhusa tano zinazoonesha wepesi aliopewa mgonjwa katika kutimiza Sala tano za faradhi.

WEPESI ALIOPEWA MGONJWA KATIKA KUTEKELEZA SWALA.

Swala ni nguzo baina yetu na mola wake. Swala ni wajibu na ni lazima kwa kila mtu kuitekeleza. Kwa wale waliopata dharura kama ugonjwa au safari wamepewa tahfifu mbalimbali. Zifuatazo ni tahfifu alizopewa mgonjwa katika kutekeleza swala.

Kutayammam. Mgonjwa amenuhusiwa kutayammam kama ugonjwa alionao hauruhusu kutumia maji. Hii inamsaidia mgonjwa katika kutekeleza swala tano za faradhi. Hii ni tahfifu aliyopewa mgonjwa katika kutimiza swala tano za faradhi.

Kuunganisha swala. Mgonjwa amenuhusiwa kuswali swala mbili kwa wakati mmoja. Anaweza kuziswali wakati wa swala ya kwanza lakini pia anaweza kuziswali wakati wa swala ya pili. Hii pia ni ~~###~~ ruhusa aliyopewa mgonjwa katika kutimiza swala tano za faradhi.

Kuswali huku akiwa amekaa. Mgonjwa ameruhusiwa kuswali huku akiwa amekaa kama hatoweza kusimama akiwa ugonjwa alionao unamzuia kusimama. Hii ni miongoni mwa ruhusa zinazoonesha wepesi aliopewa mgonjwa katika kutimiza swala tano.

Kuswali kwa kulala. Kama mgonjwa hataweza kuswali huku akiwa amekaa ameruhusiwa kuswali akiwa amelala hapo hapo kitandani au sehemu alipo- ~~lala~~ ~~kw~~ lazwa. Hii pia ni ruhusa aliyopewa mgonjwa katika kutimiza swala tano za faradhi.

Kuswali kifikra. Kama mgonjwa hataweza kuswali hata kwa kulala kwa sababu ugonjwa wake haumruhusu kufanya kitendo chochote kile basi ameruhusiwa kuswali huku akiwa anafikiria kwa kuanza kutayammam kifikra kisha kuswali kifikra. Hii pia ni ruhusa aliyopewa mgonjwa inayomsaidia kuweza kutekeleza swala tano.

Kwa ujumla hizi ndizo ruhusa tano zinazoonesha wepesi aliopewa mgonjwa katika kutimiza swala tano za faradhi na ni muhimu sana kwa muislamu kuitekeleza swala kwa hali yoyote anayoiweza kwani swali ni ufunguo wa pepo, ni amri ya Allah, na ndicho kitu kitakachotupeleka kupata mapenzi ya Allah siku ya Akhera.

Kielelezo Na 10.1: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 10.

Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi umeonesha kuwa, wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu mada ya Kusimamisha Sala nyakati za Dharura na wengine

walishindwa kubaini matakwa ya swali hilo. Aidha, baadhi ya wanafunzi hao walishindwa kujenga hoja zinazobainisha ruhusa hizo, ingawa waliashiria kuelewa swali na kuwa na ufahamu kuhusu mada husika.

Miongoni mwa wanafunzi walioshindwa kuelewa matakwa ya swali hili walieleza masharti ya utoaji wa Zakat na Sadaka na aina za Faradhi kama vile; *Faradhi ain, Faradhi kifaya, Kutoa vilivyo halalishwa, Kutoa pasina kungojea malipo na kutoa kati na kati*. Mwingine alieleza aina za hadathi zinazobainisha watu ambao hawaruhusiwi kusali kabisa ikiwa wapo katika hali hizo. Waliwataja watu walio katika: *Damu ya Mwezi (Hedhi), Nifasi (Damu ya Uzazi), na kuwa katika Janaba.* Mwingine alieleza ruhusa alizopewa mfungaji na wepesi aliopewa mgonjwa katika Sala. Mwanafunzi huyo aliandika; *Kula endapo atakuwa amefunga, Endapo atapona anahitajika kulipiza siku au mwezi ambao hajafunga mfululizo, mgonjwa ameruhusiwa*. Maelezo haya yalibainisha baadhi ya ruhusa alizopewa mgonjwa katika ibada ya Funga na si katika ibada ya Sala.

Mwingine alichanganya dhana ya kupewa wepesi na kuondolewa wajibu akidhani kwamba mgonjwa hatakiwi kusali, naye alitoa hoja zifuatazo: *Endapo mgonjwa atakuwa amezidiwa kiasi haruhusiwi kuswali, mgonjwa kama hospitali haruhusiwi kuswali, mgonjwa ambae amezidiwa kiasi hawezi kusimama au kukaa haruhusiwi kuswali.* Majibu haya yalionesha kuwa mwanafunzi hawakuelewa matakwa ya swali na alikosa maarifa kuhusu nguo ya Kusimamisha Sala, kwani ibada hii hairuhusiwi kwa Muislamu kuacha kwa sababu zozote tofauti na sababu zilizotajwa kisheria ambazo ni kuwa katika hedhi au nifasi kwa mwanamke na kurukwa na akili au kuzimia. Nje ya sababu hizo, Muislamu analazimika kudumu katika ibada hiyo maadamu bado yupo hai.

Mwanafuzi mwingine alifafanua nguzo za Uislamu badala ya ruhusa zinazoonesha wepesi aliopewa mgonjwa katika kutimiza Sala tano za faradhi. Mwanafunzi huyo alieleza kuhusu; *Kufunga Ramadhani, kuhiji Makka, Kutoa Zakat, Shaada na Kuswali swala tano.* Majibu haya hayakuwa sahihi kwa sababu hayakuakisi matakwa ya swali, hivyo ni wazi kuwa mwanafunzi huyo hakuelewa swali.

Vilevile, wanafunzi wengine walionesha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada hii ya Nguzo za Uislamu hususani kipengele cha

Kusimamisha Sala nyakati za Dharura. Wanafunzi hao walitoa hoja mbalimbali kama vile; *Kuswali rakaa zote, kuwa na udhu, kuwa na Imani na kuwafanyia wepesi wasiojiweza*. Mwingine akaandika; *Nia, Kusikiliza Qur'an na mavazi*. Hoja hizi zinaonesha kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa ya kutosha kuhusu Kusimamisha Sala nyakati za Dharura, hivyo walijibu kwa maoni yao. Kielelezo namba 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali la 10.

10. Bainisha ruhusa tano zinazoonesha wepesi aliopewa mgonjwa katika kutimiza Sala tano za faradhi.

Ni ruhusa ambazo anapewa mtu/mgonjwa wa kiislamu pale anapotakiwa kutimiza Sala tano za faradhi. Zituatazo ni:- ruhusa ambazo mgonjwa ameruhusiwa kwa ugonjwa maalumu;

Damu ya mwezi; Hii ni damu ambayo inatoka kila mwezi kutokana na siku zake na hii damu ipo kwa wasichana/wanawake walio baleghe na hapo mwanamke mwislamu hapewa ruhusa ya kutotimiza Sala zote tano za faradhi kwa ajili hiyo.

Janaba; Hii hutokea kwa wanaume ambao tayari wameshapitia ile hali ya kuwa mtu mzima hii hutokana na uchafu unaotoka mara kwa mara sehemu za siri za mwanaume na haruhusiwi akiwa kwenye hali ile kutekeleza au kutimiza Sala tano za faradhi kwa kuwa amengiliapika kila mara.

Nifasi; Ni damu inayotoka ukeni baada ya mwanamke kujifungua (damu ya uzazi) ambayo mwanamke haruhusiwi kuswali, kushika msahafu, kuingia msikitini, kutupu kaaba na kadhalika kwa kuwa atakuwa ana najisi ya damu kila muda.

Umahututi; Hii ni hali ambayo mgonjwa yuko kwenye hali ya kutojiweza (kula, kuswali, kunywa na kadhalika) huyo mtu akiwa kwenye hii hali basi mtu huyo hupewa ruhusa kwa kuwa hana ule uwezo wa kufanya chochote yupo hoi tu kitandani.

Kupunguza sadaqa; Hii ni sababu ambayo mola amesema mtu ambayo hupunguza mali au huduma inayotakiwa basi huyo mtu haruhusiwi kuzitekeleza na kuzitimiza sala zote hizo tano za faradhi kwa usahihi.

Hivyo basi; Hizo ndio ruhusa anazopewa mja anae ugua au aliyetatizwa na jambo fulani, tunamuomba mola atupe nguvu na afya na Imani tuwe nayo ya kweli kuweza kumtii na kumtumikia katika uungu wake siku zote, Inshaallah.

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.2 mwanafunzi alishindwa kubainisha ruhusa tano zinazoonesha wepesi aliopewa mgonjwa katika kutimiza Sala tano za faradhi badala yake alifafanua hali ambazo zinamzuia mtu kusali.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Katika upimaji huu mada zifuatazo zilihusika; *Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu, Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Nguzo za Uislamu, Qur'an, Sunnah na Hadithi, Bara Arab zama za Jahiliyyah, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu, Historia Katika Uislamu, Fiqh* na *Kumjua Mwenyezi Mungu (S.W)*. Uchambuzi wa takwimu za matokeo ya wanafunzi kwa mada umeonesha kuwa kiwango kizuri cha ufaulu kilikuwa katika mada ya *Kumjua Mwenyezi Mungu (77.53%).* Vile vile kulikuwa na ufaulu wa wastani katika mada za *Fiqh (56.28%), Nguzo za Uislamu (55.51%), Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu (47.71%) na Historia Katika Uislamu (37.45%).* Aidha, mada ambazo zilikuwa na ufaulu wa kiwango cha chini zilikuwa *Qur'an (15.42%), Bara Arab Zama za Jahiliyyah (11.11%),* na *Sunnah na Hadithi (6.83%)* ambazo zilipimwa katika maswali ya 6, 9 na 7 mutawalia.

Ufaulu ulikuwa wa wastani katika mada za *Fiqh, Nguzo za Uislamu, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu na Historia Katika Uislamu* ulisababishwa na wanafunzi kujibu kwa usahihi katika kipengele kimoja na kushindwa katika kipengele kingine, hali hiyo iliashiria kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika baadhi ya vipengele vya mada husika.

Aidha, ufaulu ulikuwa dhaifu katika mada za *Qur'an, Bara Arab Zama za Jahiliyyah* na *Sunnah na Hadithi* ufaulu huu dhaifu ulitokana na sababu mbalimbali kama vile; kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika, kutofuata maelekezo ya swali na kutojua matakwa ya maswali. Wanafunzi wengine walishindwa kujieleza katika baadhi ya maswali ya majibu mafupi na insha hivyo walipata alama za chini. Takwimu za ufaulu wa kila mada zimeoneshwa kwenye kiambatisho ambapo rangi nyekundu inaonesha kiwango cha chini cha ufaulu, rangi ya njano inaonesha kiwango cha wastani cha ufaulu. Kadhalika, rangi ya kijani inaonesha kiwango kizuri cha ufaulu.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu katika upimaji huu wa Kidato cha Pili (FTNA) 2022 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kilikuwa cha wastani kwa asilimia 48.77. Taarifa hii imeonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika upimaji unaofuata. Changamoto zilizojitokeza kwa wanafunzi katika kujibu maswali ni pamoja na wanafunzi kutofuata maelekezo ya swali, kushindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza, kuorodhesha majibu kwa namba au herufi kwenye swali linalohitaji kujibiwa kwa muundo wa insha au maelezo mafupi na kukosa maarifa katika mada mbalimbali hususani mada za *Qur'an, Bara Arab Zama za Jahiliyyah* na *Sunnah na Hadithi.*

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua zaidi kiwango cha ufaulu katika upimaji ujao, juhudi za ziada zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji katika mada zenye ufaulu wa chini na wastani ili kuwapa wanafunzi maarifa ya kutosha na uwezo wa kujenga hoja. Aidha, wanafunzi wanatakiwa kujengewa uwezo wa kuelewa matakwa ya maswali na kuwasilisha maarifa katika namna inayostahili. Walimu wanapaswa kutumia vitabu vya kiada (Elimu ya Dini ya Kiislamu shule za Sekondari) na ziada (Elimu ya Kiislamu kwa Posta) ili kuwapa wanafunzi maarifa stahiki.

Kwa ujumla ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu wawaongoze wanafunzi kujadili katika vikundi na kurejea muhtasari wa somo na vitabu vya kiada na ziada ili kupata maarifa ya kutosha hususani katika mada za Sunna na Hadithi, Bara Arab zama za Jahiliyyah, Qur'an na Historia katika Uislamu.

(b) Walimu wawapime wanafunzi kwa kutumia maswali yanayopima umahiri ili kuwajengea uwezo wa kubaini matakwa ya swali na namna bora ya kuwasilisha majibu hususani katika maswali ya majibu mafupi na insha.

**Kiambatisho Cha Pekee**

**Uchambuzi wa Ufaulu wa Wanafunzi Katika Mada**

<table>
<tr><th rowspan="2">Na.</th><th rowspan="2">Mada</th><th colspan="2">Ufaulu wa Kila Swali</th><th rowspan="2">Asilimia ya Wanafunzi waliopata wastani wa alama 30 au zaidi</th><th rowspan="2">Maoni</th></tr>
<tr><th>Namba ya Swali</th><th>Asilimia ya Ufaulu</th></tr>
<tr><td>1</td><td>Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Nguzo za Uislamu, Qur'an, Sunna na Hadithi, Historia Katika Uislamu.</td><td>1</td><td>94.80</td><td>94.80</td><td>Vizuri</td></tr>
<tr><td>2</td><td>Kumjua Mwenyezi Mungu</td><td>3</td><td>77.53</td><td>77.53</td><td>Vizuri</td></tr>
<tr><td>3</td><td>Fiqh</td><td>4</td><td>56.28</td><td>56.28</td><td>Wastani</td></tr>
<tr><td rowspan="2">4</td><td rowspan="2">Nguzo za Uislamu</td><td>2</td><td>63.35</td><td rowspan="2">55.51</td><td rowspan="2">Wastani</td></tr>
<tr><td>10</td><td>47.66</td></tr>
<tr><td>5</td><td>Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti Muislamu</td><td>5</td><td>47.71</td><td>47.71</td><td>Wastani</td></tr>
<tr><td>6</td><td>Historia Katika Uislamu</td><td>8</td><td>37.45</td><td>37.45</td><td>Wastani</td></tr>
<tr><td>7</td><td>Qur'an</td><td>6</td><td>15.42</td><td>15.42</td><td>Dhaifu</td></tr>
<tr><td>8</td><td>Bara Arab zama za Jahiliyyah</td><td>9</td><td>11.11</td><td>11.11</td><td>Dhaifu</td></tr>
<tr><td>9</td><td>Sunnah na Hadithi</td><td>7</td><td>6.83</td><td>6.83</td><td>Dhaifu</td></tr>
<tr><td colspan="4">Wastani wa Jumla wa Ufaulu</td><td>44.74</td><td>Wastani</td></tr>
</table>